# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MKAKATI WA KITAIFA WA UMATAIFISHAJI WA ELIMU

Oktoba, 2025

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MKAKATI WA KITAIFA WA UMATAIFISHAJI WA ELIMU

**Oktoba, 2025**

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ v

**DIBAJI** ........ vi

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ vii

**UFAFANUZI WA MANENO** ........ viii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Chimbuko ........ 2

1.3 Umataifishaji wa Elimu ........ 3

1.4 Faida za Umataifishaji ........ 3

1.5 Mbinu za Umataifishaji wa Elimu ........ 4

1.6 Mbinu Zilizotumika Kuandaa Mkakati ........ 5

1.7 Mpangilio wa Mkakati ........ 6

**SURA YA PILI** ........ 7

**2. UCHAMBUZI WA HALI YA SASA** ........ 7

2.1 Hali Ilivyo Sasa ........ 7

2.2 Uwezo ........ 8

2.3 Mapungufu ........ 9

2.4 Fursa ........ 9

2.5 Changamoto ........ 10

**SURA YA TATU** ........ 11

**3. DIRA, DHIMA NA MALENGO** ........ 11

3.1 Dira ........ 11

3.2 Dhima ........ 11

3.3 Malengo ya Mkakati ........ 11

3.3.1 Lengo la Jumla ........ 11

3.3.2 Malengo Mahususi ........ 11

**SURA YA NNE** ........ 13

**4. MAENEO, MALENGO NA MIKAKATI YA UMATAIFISHAJI WA ELIMU** ........ 13

4.1 Umataifishaji wa Mitaala ........ 13

4.1.1 Elimumsingi ..... 13
4.1.2 Elimu ya juu ..... 14
4.2 Programu za Ushirikiano na Taasisi za Elimu Nje ya Nchi ..... 15
4.2.1 Elimu ya juu ..... 15
4.3 Udahili na Uandikishaji wa Wanafunzi Ndani ya Nchi ..... 16
4.3.1 Elimumsingi ..... 16
4.3.2 Elimu ya juu ..... 17
4.4 Udahili na Uandikishaji wa Wanafunzi Kusoma Nje ya Nchi ..... 18
4.4.1 Elimumsingi ..... 18
4.4.2 Elimu ya juu ..... 19
4.5 Kuajiri Walimu, Wanataaluma na Wataalamu wengine kutoka Nje ya Nchi 19
4.5.1 Elimumsingi ..... 20
4.5.2 Elimu ya Juu ..... 20
4.6 Mabadilishano ya Wanafunzi, Walimu, Wanataaluma na Wataalamu wengine ..... 21
4.6.1 Elimumsingi ..... 21
4.6.2 Elimu ya juu ..... 22
4.7 Mashirikiano katika Elimu, Stadi, Utafiti na Ubunifu ..... 22
4.7.1 Elimumsingi ..... 23
4.7.2 Elimu ya juu ..... 23
4.8 Taasisi za Elimu Nje ya Nchi ..... 24
4.8.1 Elimumsingi ..... 24
4.8.2 Elimu ya juu ..... 24
4.9 Taasisi za Elimu za Nje ndani ya Nchi ..... 25
4.9.1 Elimumsingi ..... 25
4.9.2 Elimu ya juu ..... 26
4.10 Lugha ya Kiswahili ..... 26
4.10.1 Malengo ..... 27
4.10.2 Mikakati ..... 27
4.11 Matumizi ya Balozi za Ndani na Nje ya Nchi ..... 27
4.11.1 Malengo ..... 27
4.11.2 Mikakati ..... 28

4.12 Taasisi za Uwakala wa Elimu Ndani ya Nchi ........ 28
4.12.1 Malengo ........ 28
4.12.2 Mikakati ........ 28
4.13 Udahili wa Wanafunzi Kutoka Nchi Zenye Majanga ........ 29
4.13.1 Malengo ........ 29
4.13.2 Mikakati ........ 29
**SURA YA TANO ........ 30**
**5. MPANGILIO WA KITAASISI NA MAJUKUMU ........ 30**
5.1 Majukumu ya Serikali ........ 30
5.2 Majukumu ya Taasisi za Elimu ........ 31
5.3 Majukumu ya Taasisi Rekebu ........ 31
5.4 Majukumu ya Balozi ........ 32
5.5 Majukumu ya Taasisi za Uwakala ........ 32
**SURA YA SITA ........ 33**
**6. UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 33**
**Marejeo ........ 54**

# ORODHA YA MAJEDWALI

JEDWALI NA. 1: Jedwali la Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu ..... 33

JEDWALI NA. 1 (a): ELIMUMSINGI ..... 33

JEDWALI NA. 1 (b): ELIMU YA JUU ..... 41

JEDWALI NA. 1 (c): MASUALA MTAMBUKA ..... 50

# DIBAJI

Umataifishaji wa elimu ni nyenzo muhimu katika kukuza na kuendeleza elimu na maendeleo ya Taifa. Umataifishaji wa elimu unaleta manufaa mbalimbali katika taifa. Kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi wa kigeni na ushirikiano kati ya taasisi za ndani na nje ya nchi kunaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya fedha za kigeni, huku pia ikiimarisha hadhi na ubora wa elimu nchini katika viwango vya kimataifa. Aidha, utalii wa elimu unachangia kuongeza mapato, huku ukitoa fursa kwa wanafunzi kupata ufahamu mpana na maarifa kuhusu masuala mbalimbali ya kimataifa, na kuleta mwingiliano chanya wa mila na tamaduni kutoka nchi mbalimbali. Kuimarishwa kwa mitaala yenye ubora wa viwango vya kimataifa pia kunasaidia kuongeza ushindani wa kimataifa wa taasisi za elimu na kuleta ulinganifu wa elimu katika soko la dunia. Hatua hizi siyo tu zinawasaidia wahitimu kwa kuwapa soko la ajira lililopanuka kimataifa, lakini pia huchochea mahusiano ya kidiplomasia kati ya nchi na nchi, ambayo yanaboresha zaidi mazingira ya elimu na ajira kwa wafanyakazi wa taasisi hizi.

Ili kufikia malengo ya umataifishaji, ni lazima mfumo wa elimu na mafunzo uzingatie viwango vya kimataifa. Mfumo huo wa elimu unatakiwa kutoa elimu na mafunzo yenye ubora unaokubalika na kutambulika kitaifa, kikanda, na kimataifa. Hivyo, taasisi za elimu hazina budi kuweka malengo ya kufikia vigezo na viwango vya kimataifa. Mfano wa viwango vya kimataifa, kwa upande wa vyuo vikuu, ni kuwa na angalau asilimia tano ya idadi ya wanafunzi wa nje ya nchi. Aidha, kwa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kufikia viwango vya kimataifa, moja ya vigezo ni kuanzisha na kutekeleza mashirikiano na taasisi za kimataifa. Mkakati huu wa umataifishaji umeandaliwa mahsusi kutoa mwelekeo na namna ya kuwezesha na kufanikisha umataifishaji wa elimu Tanzania.

Walengwa wakubwa wa Mkakati huu ni wadau wote wa elimu zikiwemo taasisi za elimu na ithibati, wanafunzi, wazazi, taasisi za dini na sekta binafsi. Ni matumaini yangu kwamba, utekelezaji wa Mkakati huu utatoa mchango mkubwa katika jitihada za Serikali za kuendeleza elimu kwa viwango vya kimataifa.



Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AAU | Association of African Universities |
| AERC | African Economic Research Consortium |
| CECED | Centre for Economics and Community Economic Development |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| EAC | East African Community |
| IUCEA | Inter- University Council for East Africa |
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| NORAD | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| OR-MUUUB | Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| SADC | The Southern African Development Community |
| SARUA | Southern African Regional Universities Association |
| SWISSAID | Switzerland Aid |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| USAID | United States Agency for International Development |
| WB | World Bank |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# UFAFANUZI WA MANENO

| | |
|---|---|
| Balozi | Inamaanisha Balozi za Tanzania nje ya nchi na Balozi za nchi za nje nchini. |
| Njia mseto | Ujifunzaji na ufundishaji kwa njia ya uso kwa uso na mtandao |
| Elimumsingi | Inajumuisha elimu ya awali, msingi na sekondari |
| Elimu ya juu | Inajumuisha elimu ya ualimu, ufundi, mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu. |
| Taasisi za Elimu | Inajumuisha Taasisi za Elimumsingi na Elimu ya juu. |
| Majanga | Inamaanisha matukio makubwa ya hatari yanayoikumba nchi au jamii ikiwemo migogoro ya kisiasa, matetemeko ya ardhi, njaa, afya na uchumi. |
| Wizara za kisekta | Wizara zote zitakazo husika kwenye utekelezaji wa mkakati |

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Kulingana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 na Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo ya Taifa 2011/12 hadi 2024/25 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) sekta ya elimu na mafunzo inatarajiwa kuongeza maendeleo ya rasilimaliwatu kwa kutayarisha Watanzania wenye ujuzi, stadi na umahiri ili kuliletea taifa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Chama cha Mapinduzi kupitia ilani yake ya 2025 - 2030 imetoa mwongozo wa kuimarisha mfumo wa elimu ili uweze kuzalisha wataalamu mahiri wenye uwezo katika sayansi, teknolojia, ufundi, stadi za kazi na nyanja nyingine.

Kutokana na mwingiliano wa kiuchumi, kisiasa, na kijamii baina ya Tanzania, nchi marafiki, na jumuiya za kikanda na kimataifa, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania 2014, toleo la mwaka 2023, katika eneo ubora wa elimu, Wizara imeweka lengo la kuboresha mitaala ya Elimu na Mafunzo ili kukidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi na kuhimili ushindani. Katika lengo hili tamko namba **3.1.1.1** linaeleza kuwa *Serikali itahakikisha kuwapo kwa mitaala bora katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo inayoendana na wakati na inayozingatia mahitaji ya Taifa na ulimwengu wa kazi*. Aidha, makubaliano ya kikanda na kimataifa yanasukuma umataifishaji wa elimu, ikiwa ni pamoja na kufanya ulinganifu wa masomo, programu, na vigezo vya uandikishaji na udahili katika nchi wanachama.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kutekeleza majukumu yake, imezingatia Malengo Endelevu ya Dunia kuhusu elimu jumuishi yenye ubora na kutolewa kwa usawa; Tamko la Haki za Binadamu kuhusu haki ya elimu kwa wote; Ajenda ya Afrika ya 2063 kuhusu elimu jumuishi kwa maendeleo endelevu; Itifaki ya Soko la Pamoja Ibara ya 11 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki ya Elimu na Mafunzo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika zinatoa mwongozo wa uwepo wa uwiano kati ya mifumo ya elimu na mitaala kwa nchi wanachama.

Ili kufikia malengo na miongozo hiyo, ni lazima mfumo wa elimu na mafunzo utoe fursa za kutosha kwa watu wengi zaidi kuelimika na kuendelea kujielimisha. Mfumo huo wa elimu unatakiwa kutoa elimu na mafunzo yenye ubora unaokubalika na kutambulika kitaifa, kikanda, na kimataifa. Hivyo, taasisi za elimu hazina budi kuweka malengo ya kufikia vigezo na viwango vya kimataifa. Mfano wa viwango vya kimataifa, kwa upande wa vyuo vikuu, ni kuwa na angalau asilimia tano ya idadi ya wanafunzi wa nje ya nchi. Aidha, kwa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kufikia viwango vya kimataifa, moja ya vigezo ni kuanzisha na kutekeleza mashirikiano na taasisi za kimataifa.

Kwa sasa, Tanzania inakabiliwa na uwepo wa idadi ndogo ya wanafunzi na wataalamu wa nje ya nchi na upatikanaji hafifu wa ufadhili na fursa za masomo kwa Watanzania.

Hivyo, kuna haja ya kuweka mkakati wa kukuza umataifishaji wa elimu ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kutoka nje ya nchi, kuongeza fursa za masomo nje ya nchi na kuimarisha ushindani wa wahitimu kikanda na kimataifa. Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu Tanzania wa 2024 - 2029 unatoa mwongozo wa kuwezesha taasisi za elimu kutoa elimu yenye kukidhi vigezo na viwango vya kikanda na kimataifa.

## 1.2 Chimbuko

Elimu ni chombo muhimu sana katika kuhakikisha taifa linapata raia wenye uwezo wa kuchangia maendeleo ya nchi. Tangu Tanzania ilipopata uhuru mwaka 1961, serikali imechukua hatua mbalimbali katika nyakati tofauti za kurekebisha na kuimarisha mifumo ya elimu ili kufikia malengo ya maendeleo kama yanavyoainishwa katika mipango mbalimbali. Utekelezaji wa mipango hiyo umechangia kwa kiasi kikubwa, mageuzi ya kiwango cha juu katika sekta ya elimu.

Mageuzi katika sekta ya elimu yanachangia uboreshwaji wa taasisi za elimu nchini, hivyo kuvutia wanafunzi na wataalamu kutoka nchi za kigeni. Sambamba na hilo, maendeleo ya kiteknolojia, ikiwa ni pamoja na kuboreshwa kwa upatikanaji wa mitandao na majukwaa ya kujifunza kidijitali, yamewezesha ushirikiano wa kimataifa na ufikiaji wa rasilimali za elimu za kimataifa. Zaidi ya hayo, kuongezeka kwa mahitaji ya elimu bora yenye viwango vya kimataifa kumesukuma taasisi za Tanzania kutafuta ufadhili na ubia wa kimataifa. Mambo haya kwa pamoja yanakuza mazingira yanayofaa kwa mfumo wa elimu wa Tanzania kuwa na sura ya kimataifa, na hivyo kuongeza ubora na ushindani wa elimu kimataifa.

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 imebainisha wazi kwamba Tanzania inapaswa kujizatiti kujenga ubunifu, ustadi, na elimu bora ili kukabiliana na changamoto za kimaendeleo na kushindana kikamilifu kikanda na kimataifa. Kwa kuzingatia dhamira hii, Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 toleo la mwaka 2023 inalenga kuiwezesha nchi kuwa na elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora vinavyotambulika kitaifa, kikanda, na kimataifa.

Kwa kuzingatia mwelekeo wa Dira na malengo ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 toleo la 2023, Serikali ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali katika nyakati tofauti za kurekebisha na kuimarisha mifumo ya elimu ili kufuata maendeleo ya elimu duniani na kufikia malengo ya maendeleo kama inavyoainishwa kwenye Dira, Sera, na Mipango ya Serikali.

Ukuaji wa kasi wa maendeleo ya sayansi, teknolojia, na utandawazi duniani umechangiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya ubora wa elimu, utafiti, na mafunzo kwa ujumla. Ili Tanzania iweze kuendana na kasi ya ukuaji wa elimu, utafiti, na mafunzo katika viwango vya kikanda na kimataifa, ni muhimu kuandaa mikakati na mipango itakayowezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mkakati huu unalenga kuwezesha elimu inayotolewa Tanzania kuwa na sura yenye maudhui ya kimataifa, ambayo itatoa fursa kwa wanafunzi na wataalamu kujifunza pia kunufaika na maendeleo ya elimu, utafiti, na mafunzo kimataifa. Mkakati huu vilevile utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha elimu kwa nchi zingine za kikanda na kimataifa.

## 1.3 Umataifishaji wa Elimu

Dhana ya umataifishaji wa elimu inahusisha hali ya kuwepo kwa utaratibu ambao unatoa fursa kwa elimu inayotolewa kuwa na viwango vya kikanda na kimataifa. Kwa mujibu wa tafiti na rejea za machapisho mbalimbali, umataifishaji unatekelezwa kupitia makundi makuu mawili; umataifishaji wa ndani ya nchi na umataifishaji wa nje ya nchi.

Umataifishaji wa ndani ya nchi unahusisha maandalizi ya mitaala na mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji ili kuvutia wanafunzi, walimu, wakufunzi, wanataaluma, watafiti na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi. Aidha, umataifishaji huu wa ndani ya nchi unajumuisha uandaaji wa mbinu na vifaa vya TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa elimu kwa njia ya mtandao. Vilevile, umataifishaji wa ndani unahusisha maandalizi na uimarishaji wa mifumo, mitaala na mazingira ya kujifunzia kwa ngazi zote za elimu ili ziweze kupokea, kuandikisha na kudahili wanafunzi kutoka nje ya nchi na pia kuvutia wataalamu kutoka nje ya nchi. Umataifishaji nje ya nchi unajumuisha uandikishaji na udahili wa wanafunzi, ushirikiano wa taasisi za ndani na nje ya nchi, mabadilishano ya wataalamu nje ya nchi pamoja na kuanzisha shule, vyuo na kampasi za taasisi za elimu nje ya nchi.

Kwa mantiki hii, taasisi za elimu zina wajibu wa kujenga na kuendeleza dhana ya umataifishaji na kuimarisha ushindani katika ngazi ya kimataifa ili kuongeza umahiri wa taasisi katika taaluma na tafiti kimataifa. Vilevile, umataifishaji wa elimu ni chanzo cha mapato ya fedha za ndani na za kigeni.

## 1.4 Faida za Umataifishaji

Faida za Umataifishaji ni pamoja na zifuatazo: -

i. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kupitia uandikishaji na udahili wa wanafunzi wa kigeni na ushirikiano kati ya taasisi za ndani na nje ya nchi;

ii. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kupitia utalii wa elimu nchini;

iii. Kuongezeka kwa sifa, hadhi na viwango vya ubora wa elimu kimataifa katika taasisi za elimu;

iv. Kuwepo kwa mitaala ya elimu yenye ubora na viwango vya kimataifa;

v. Kuongezeka kwa maarifa na mwingiliano chanya wa mila, desturi na tamaduni za nchi nyingine;

vi. Kuongezeka kwa ufahamu na uzoefu kwa wanafunzi kuhusu masuala mbalimbali ya kimataifa;

vii. Kuchochea mahusiano ya kidiplomasia kati ya nchi na nchi;

viii. Kuongeza ushindani na ulinganifu wa viwango vya elimu kimataifa kwa taasisi za elimu; na

ix. Kuongeza soko na wigo wa fursa za ajira kwa wahitimu na wafanyakazi wa taasisi za elimu.

## 1.5 Mbinu za Umataifishaji wa Elimu

Mbinu zinazoweza kutumika kufanikisha umataifishaji wa elimu ni pamoja na:

i. Kutangaza na kueneza programu na huduma zinazotolewa na taasisi za elimu kitaifa, kikanda na kimataifa;

ii. Kuongeza vigezo vya udahili ili kukidhi viwango vya kimataifa katika ngazi ya shule za awali na msingi, sekondari, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi hadi elimu ya juu;

iii. Kuboresha mifumo ya ujifunzaji na ufundishaji hususani matumizi ya TEHAMA;

iv. Kuboresha mazingira na miundombinu ya elimu kuwa rafiki, wezeshi na ya kimataifa;

v. Kuongeza ubora wa bunifu na tafiti kufikia viwango vya kimataifa;

vi. Kuboresha mitaala na programu za masomo ziendane na viwango vya kimataifa;

vii. Kuwepo kwa wataalamu wa viwango vya kimataifa;

viii. Kuingia makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi.

ix. Kuandaa fursa au makongamano ya utalii wa kimasomo (academic tourism)

Kwa kuzingatia mbinu na faida zilizoelezwa hapo juu, Mkakati huu utajumuisha mambo yafuatayo: -

i. Kuandaa mitaala inayoendana na mahitaji ya elimu kitaifa, kikanda na kimataifa;

ii. Kujenga uwezo wa lugha, mbinu na vifaa vya ujifunzaji na ufundishaji kulingana na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa;

iii. Kuongeza fursa na idadi ya wanafunzi watakaosoma ndani na nje ya nchi;

iv. Kuongeza vivutio kwa wanafunzi wa kigeni kuja kusoma nchini;

v. Kupeleka wataalamu nje ya nchi kwa ajili ya kukuza ujuzi;

vi. Kuwepo walimu, wanataaluma, watafiti na wataalamu wengine kutoka nchi za nje kufanya kazi katika taasisi za elimu nchini; na

vii. Kuboresha miundombinu ya ujifunzaji, ufundishaji na utafiti.

## 1.6 Mbinu Zilizotumika Kuandaa Mkakati

Mkakati wa umataifishaji umeandaliwa kupitia mchakato wa kina wa tafakuri na mashauriano mbalimbali. Aidha, mbinu mbalimbali zilitumika kuandaa Mkakati huu, ikiwemo kupitia nyaraka mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa; kuhusisha na kukusanya maoni ya wadau na kufanya ulinganifu na taasisi za elimu nje ya nchi.

**i. Mapitio ya Nyaraka**

Wizara iliunda kikosi kazi kilichopitia nyaraka mbalimbali ikiwemo, miongozo ya umataifishaji, makubaliano na taarifa mbalimbali za elimu nchini, kikanda na kimataifa. Aidha, kikosi kazi kilipitia Sera ya Elimu ya mwaka 2014 toleo la 2023, kitabu cha mwongozo cha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Sera ya Umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Sera ya Umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Nyaraka nyingine zilizopitiwa ni pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Sera ya Umataifishaji ya Afrika Kusini ya mwaka 2019, Mkakati wa Muungano wa Vyuo vya Afrika (AAU) wa mwaka 2020-2025, Mkakati wa Chama cha Vyuo Vikuu vya Kanda ya Afrika Kusini wa mwaka 2008-2012 na mwaka 2024-2028, Itifaki ya kuanzishwa kwa soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2008.

Aidha, nyaraka nyingine zilizopitiwa ni pamoja na Itifaki ya elimu na mafunzo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya 2000 na Mkakati wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki wa 2021-2026. Nyaraka za kimataifa zilizopitiwa kama marejeo ni pamoja na Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu ya Juu wa Finland (2009–2015) na Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu ya Juu wa Jamhuri ya Czech (2021).

**ii. Ukusanyaji wa Maoni ya Wadau**

Maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu na umataifishaji yalikusanywa, yakafanyiwa uchambuzi na kutumika kwenye uandaaji wa Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu Tanzania. Utaratibu wa ukusanyaji wa maoni ulihusisha warsha mbili tofauti zilizojumuisha makundi saba ya wadau; wadau kutoka vyuo vikuu na vyuo vya kati, taasisi za uwakala wa elimu, wadhibiti ubora wa elimu, mabaraza ya

kitaaluma, Chama cha Wamiliki wa Shule za Binafsi, idara mbalimbali za serikali na Jumuiya ya Vyama vya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Ukusanyaji wa maoni uliendeshwa kwa Wizara kufanya wasilisho la Mkakati na wadau kuuliza maswali ili kupata ufafanuzi. Aidha, wadau wote walipewa fursa ya kujadili Rasimu ya Mkakati kwa makundi. Mwisho, wadau waliwasilisha maoni na maboresho kwa mazungumzo na kwa maandishi. Maoni yaliyopokelewa yalitumika kuboresha na kuandaa Mkakati unaojumuisha maoni hayo.

**iii. Ufanyaji wa Ulinganifu**

Ili kuandaa mkakati huu, wizara ilifanya ulinganifu wa miundo na uendeshaji wa umataifishaji katika taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi. Kwa upande wa uendeshaji wa umataifishaji kitaifa, wizara ilifanya ulinganifu kwa ngazi za wizara na kitaifa katika nchi za Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Finland na Czech Republic. Aidha, ulinganifu ulifanywa kupitia nyaraka mbalimbali zinazopatikana kwenye tovuti za taasisi za kimataifa.

## 1.7 Mpangilio wa Mkakati

Mkakati huu una jumla ya sura sita. Sura ya kwanza ni utangulizi, ambapo umuhimu wa kuwa na Mkakati wa Umataifishaji na mbinu zilizotumika kuuandaa zimeelezwa. Uchambuzi wa uwezo, udhaifu, changamoto na fursa umejumuishwa kwenye sura ya pili. Sura ya tatu inaelezea umuhimu, dira, dhima na malengo ya mkakati wakati maeneo ya kimkakati, malengo na mikakati yameelezwa kwenye Sura ya Nne. Majukumu ya Serikali na taasisi za umma na binafsi yameelezwa katika Sura ya Tano na mkakati unakamilishwa kwa maelezo kuhusu ufuatiliaji na tathmini katika sura ya sita.

# SURA YA PILI

## 2. UCHAMBUZI WA HALI YA SASA

### 2.1 Hali Ilivyo Sasa

Umataifishaji wa elimu ni njia muhimu na ya kimkakati ya kukuza na kuleta mabadiliko ya elimu na mafunzo duniani. Msukumo wa utekelezaji wa dhana ya umataifishaji ulianza na kukua katika miaka ya karibuni kutokana na ukuaji wa utandawazi na utangamano wa kimataifa. Umataifishaji wa elimu katika bara la Marekani umefanikiwa zaidi katika programu za masomo nje ya nchi, udahili wa wanafunzi wa kigeni na umataifishaji wa wanataaluma.

Kwa upande wa bara la Ulaya, uwepo wa mfumo wa pamoja wa ithibati na udhibiti wa ubora wa elimu, umewezesha udahili wa wanafunzi katika nchi yoyote ya Ulaya. Aidha, uratibu wa mabadilishano ya wanafunzi, wanataaluma na wafanyakazi kati ya mataifa ya Ulaya na nchi nyingine duniani ni namna nyingine muhimu ya umataifishaji barani Ulaya. Katika bara la Asia, umataifishaji umechochewa na maendeleo ya elimu na maboresho ya ubora wa elimu.

Dhana ya umataifishaji ni moja ya masuala muhimu na ya kipaumbele katika Jumuiya za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Ili kukuza na kuimarisha upatikanaji wa elimu na ujuzi katika ngazi zote, jumuiya hizo, kupitia itifaki mbalimbali, zimeanzisha mifumo ya udhibiti wa ubora wa elimu katika ngazi zote. Mfano wa mifumo hiyo ni pamoja na makubaliano ya kulifanya eneo la Afrika Mashariki kuwa eneo moja la Elimu ya Juu mwaka 2017, kuanzishwa kwa mfumo wa pamoja wa ithibati na udhibiti wa Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuanzishwa kwa mfumo wa pamoja wa ithibati na udhibiti wa Elimu ya Juu kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Malengo ya jumla ya kuanzishwa kwa mifumo hiyo ni kuhuisha viwango vya ubora wa elimu inayotolewa na kuwezesha wananchi wa Jumuiya hizo kuweza kutangamana na hivyo kupanua fursa za kubadilishana wataalamu na ujuzi na hivyo kukuza na kuimarisha ustawi wa kiuchumi wa nchi wanachama.

Uwepo wa mifumo hiyo ni fursa muhimu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukuza umataifishaji wa elimu katika ngazi zote. Kwa sasa, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na taasisi za elimu, tafiti na mawakala wa elimu imekuwa ikiratibu na kutekeleza mchakato wa umataifishaji wa elimu katika ngazi mbalimbali. Juhudi hizi ni pamoja na fursa za ufadhili kwa watanzania kusoma nje ya nchi, kuajiri wataalamu kutoka nje ya nchi pamoja na kuandaa programu za masafa na kuanzishwa kwa mfumo mseto.

Ili kushiriki kikamilifu katika umataifishaji, baadhi ya taasisi za elimu nchini zimeanzisha dawati, vitengo na kurugenzi zinazosimamia masuala ya umataifishaji. Vitengo au kurugenzi hizo zimepewa majukumu ya kuratibu udahili wa wanafunzi kutoka nje ya nchi, upatikanaji na utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano kati ya chuo na washirika wa maendeleo na kuratibu majadiliano ya umataifishaji vyuoni.

Katika Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Serikali kupitia mradi wa Kukuza Ujuzi na Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki ilianzisha vituo vya Umahiri vya Afrika Mashariki katika maeneo ya nishati jadidifu (Chuo cha Ufundi Arusha), usafiri wa anga (Chuo cha Usafirishaji), Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam) na uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi (Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na kampasi ya Mwanza).

Kwa upande wa Elimu Msingi, baadhi ya shule binafsi na baadhi ya shule za Serikali zimeanzisha madawati yanayoratibu programu za ushirikiano kati ya shule hizo na taasisi za nje. Baadhi ya programu zinazotekelezwa katika ngazi hii ni pamoja na kubadilishana walimu na wanafunzi pamoja na kufanya ziara za mafunzo.

Matokeo ya juhudi hizo ni kuongezeka kwa idadi ya ushirikiano kati ya taasisi za ndani na taasisi za nje, pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, idadi ya mashirikiano na udahili wa wanafunzi kutoka nje ya nchi ni ndogo ikilinganishwa na ukubwa wa sekta ya elimu katika ngazi zote. Hivyo kuna haja ya kuweka mikakati itakayowezesha taasisi za elimu kuongeza mashirikiano, udahili na ajira za wataalamu kutoka nje ya nchi.

Hata hivyo, ili kujenga mkakati imara wa umataifishaji, ni muhimu kufanya uchambuzi wa kina kuhusu uwezo, udhaifu, fursa na vikwazo vya umataifishaji wa elimu nchini. Lengo la uchambuzi huu ni kubainisha uwezo, udhaifu, fursa na vikwazo vilivyopo ili kuandaa mkakati unaokidhi mahitaji ya sasa na baadae.

## 2.2 Uwezo

lli kuwezesha umataifishaji wa elimu nchini, uwezo ufuatao umebainishwa: -

i. Kuwepo kwa uongozi imara katika ngazi zote;

ii. Kuwepo kwa sera na mipango ya kuboresha elimu nchini;

iii. Kuwepo kwa mfumo wa ulinganifu wa sifa za kitaalamu nchini;

iv. Kuwepo kwa sera rafiki ya uwekezaji nchini;

v. Kuwepo kwa amani, utulivu na dhamira ya kisiasa;

vi. Kuwepo kwa wataalamu waliopata mafunzo katika mataifa ya nje ya nchi;

vii. Kuwepo kwa vituo mahiri vya utafiti na mafunzo katika taasisi mbalimbali nchini;

viii. Kutumika kwa eneo la kijiografia la Tanzania kama kitovu cha utafiti na mafunzo;

ix. Kuwepo kwa vivutio vya utalii nchini;

x. Kuongezeka kwa taasisi zenye sifa na viwango vya kimataifa;

xi. Kuwepo kwa ongezeko la umahiri na ubobezi katika lugha ya Kiswahili;

xii. Kuwepo kwa madawati ya umataifishaji katika baadhi ya shule za awali na msingi na sekondari;

xiii. Kuwepo kwa uwekezaji na ujenzi wa majengo mapya ya kufundishia na kujifunzia;

xiv. Kuwepo kwa Balozi za Tanzania nje ya nchi;

xv. Kuwepo kwa taasisi za uwakala wa elimu; na

xvi. Kuwepo kwa taasisi rekebu zinazofanya ulinganifu nchini katika ngazi ya Msingi, sekondari na elimu ya juu.

## 2.3 Mapungufu

Pamoja na uwezo ulioelezwa hapo juu, udhaifu ufuatao umebainishwa: -

i. Uelewa hafifu wa dhana na tija ya umataifishaji kwa taasisi za elimu nchini;

ii. Upungufu wa rasilimali fedha na wataalamu wa umataifishaji;

iii. Kuwepo kwa miundombinu hafifu ya ujifunzaji, ufundishaji na utafiti;

iv. Kutokuwepo kwa miundombinu rafiki katika taasisi za elimu kwa ajili ya umataifishaji;

v. Uelewa mdogo wa elimu kama biashara;

vi. Uhamasishaji mdogo wa kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika elimu;

vii. Kuwepo kwa urasimu wakati wa uchambuzi na uhakiki wa sifa na vyeti vya kitaaluma kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi; na

viii. Urasimu wa kisheria na kikanuni kuhusu ajira za wataalamu kutoka nje ya nchi.

## 2.4 Fursa

Pamoja na mapungufu hayo, fursa zifuatazo zimebainishwa: -

i. Kuwepo kwa mahusiano ya kihistoria kati ya Tanzania na nchi za kusini mwa Afrika (Namibia, Afrika Kusini, Msumbiji nk);

ii. Kuwepo kwa mahusiano kati ya taasisi za elimu na mashirika ya kimataifa;

iii. Kuwepo kwa miradi inayotekelezwa kupitia wadau wa maendeleo kutoka nje ya nchi;

iv. Uanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi wanachama wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, na jumuiya zingine za kikanda na kimataifa;

v. Kupanuka kwa utandawazi duniani;

vi. Kukua na kuboreshwa kwa njia mbalimbali za mawasiliano duniani;

vii. Kuwepo kwa nchi zinazoshindwa kusimamia na kuendesha shughuli za elimu kwa utulivu kutokana na majanga au vita;

viii. Uwepo wa Balozi za nchi za nje nchini; na

ix. Kuwepo kwa taasisi zilizo tayari kufadhili elimu duniani.

## 2.5 Changamoto

Hata hivyo, zipo changamoto zilizojitokeza katika kuandaa mkakati na mpango wa utekelezaji wa mwongozo huu. Changamoto zifuatazo zilibainishwa: -

i. Kutokuwepo kwa ulinganifu wa mifumo ya elimu kati ya Tanzania na nchi nyingine hivyo kuwanyima sifa za kujiunga na elimu ya juu wanafunzi kutoka baadhi ya nchi;

ii. Gharama kubwa za ufadhili wa wanafunzi na wataalamu kutoka nje ya nchi;

iii. Majanga ya asili kama mafuriko na majanga mengine yanayoharibu miundombinu na mifumo ya elimu nchini na nje ya nchi;

iv. Kutofautiana kwa vipindi vya mihula ya masomo kati ya taasisi za elimu ~~nchini~~ Tanzania na nchi nyingine;

v. Kupishana kwa taratibu za udahili wa wanafunzi wa kigeni katika taasisi za elimu nchini;

vi. Kupishana kwa viwango na miundo ya ada za masomo duniani;

vii. Mazingira ya kusomea na kuishi yasiyo rafiki, ikiwemo huduma za malazi na upatikanaji wa huduma za afya;

viii. Kutokuwepo kwa programu za masomo zenye kuvutia wanafunzi wa kigeni; na

ix. Kuwepo kwa miundombinu na vifaa vya utafiti visivyokidhi viwango vya kimataifa.

# SURA YA TATU

## 3. DIRA, DHIMA NA MALENGO

Msingi wa Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu ni kuboresha elimu ya Tanzania kuendana na viwango vya kimataifa. Mkakati huu unaongozwa na Dira, Dhima na Malengo yafuatayo: -

### 3.1 Dira

Kuwa na wataalamu wenye umahiri na ubunifu wa viwango vya kimataifa.

### 3.2 Dhima

Kuongeza ubora wa elimu, mafunzo na tafiti kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata wataalamu wenye umahiri na ubunifu wa viwango vya kimataifa kwa maendeleo ya nchi.

### 3.3 Malengo ya Mkakati

Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu utakuwa na malengo ya jumla na mahususi kama ifuatavyo:

#### 3.3.1 Lengo la Jumla

Kuwekeza kwenye umataifishaji wa elimu na tafiti ili kuandaa wahitimu na watafiti wenye maarifa, stadi, ujuzi na umahiri unaokidhi viwango na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

#### 3.3.2 Malengo Mahususi

Yafuatayo ni malengo mahususi: -

i. Kuwa na mitaala na programu za masomo zenye viwango vya kimataifa katika ngazi zote za elimu;

ii. Kuwa na wahitimu waliondaliwa kupitia ujifunzaji na ufundishaji wa viwango vya kimataifa katika ngazi zote za elimu;

iii. Kuwa na ongezeko la uandikishaji na udahili wa wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi katika ngazi zote za elimu;

iv. Kuwa na wataalamu na watafiti wenye maarifa, ujuzi, ubobezi na uzoefu wa viwango vya kimataifa;

v. Kuwa na wataalamu na watafiti wabobezi wa kimataifa kutoka taasisi za nje ya nchi na wa nchini kwenda nje ya nchi;

vi. Uwepo wa mahusiano ya kikanda na kimataifa katika elimu na tafiti;

vii. Uwepo wa mazingira na miundombinu bora katika taasisi za elimu inayowezesha umataifishaji;

viii. Uwepo wa fursa za utalii wa elimu nchini; na

ix. Uwepo wa mazingira na huduma zinazozingatia lugha, mila, desturi na tamaduni za mataifa mengine.

# SURA YA NNE

## 4. MAENEO, MALENGO NA MIKAKATI YA UMATAIFISHAJI WA ELIMU

Malengo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) ni kujenga umataifishaji endelevu katika ngazi zote za elimu kwa kutoa miongozo na mikakati inayozingatia ujumuishi na usawa wa kijinsia. Ili kufikia malengo haya, wizara itaangazia mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mazingira na mitaala inayowezesha ujifunzaji na ufundishaji wa viwango vya kimataifa.

Mkakati wa Umataifishaji umezingatia mahitaji katika ngazi zote. Katika ngazi ya awali, msingi, na sekondari, umataifishaji unahusisha kutoa elimu inayokidhi viwango vya kimataifa, kuwafanya wanafunzi wa ndani kuwa na uwezo wa kusoma nje ya nchi na wanafunzi wa nje kusoma ndani ya nchi. Kwa upande wa elimu ya juu, umataifishaji unawawezesha wahitimu kuwa na stadi, ujuzi, na maarifa ya viwango vya kimataifa na hivyo kukuza na kuimarisha utangamano na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

Katika Mkakati huu, malengo na mikakati ya umataifishaji wa elimu yamegawanyika katika ngazi mbili, Elimumsingi na elimu ya juu. Yafatayo ni maeneo ya kimkakati yakiwa na malengo na mikakati ya utekelezaji:-

### 4.1 Umataifishaji wa Mitaala

Umataifishaji wa mitaala unajumuisha dhana, maudhui na mwingiliano wa kijamii wa kimataifa katika ujifunzaji na ufundishaji. Aidha, umataifishaji wa mitaala, unajumuisha malengo na namna ya tathmini za ufundishaji, huduma za usaidizi wa programu za masomo na matokeo ya ujifunzaji na ufundishaji.

#### 4.1.1 Elimumsingi

Katika ngazi hii Mkakati unajumuisha elimu ya awali, msingi na sekondari.

#### 4.1.1.1 Malengo

i. Mitaala ya Elimumsingi yenye kuandaa wahitimu wa elimu wenye stadi, ujuzi, maarifa na utaalamu shindani kitaifa, kikanda na kimataifa kuboreshwa;

ii. Wanafunzi toka nje ya nchi kuja kusoma nchini kupitia mitaala ya Elimumsingi kuongezeka; na

iii. Taasisi za Elimumsingi kutoka nje ya nchi na taasisi za ndani kushirikiana kuandaa na kutekeleza mitaala.

#### 4.1.1.2. Mikakati

i. Kusimamia utekelezaji wa mitaala ya taifa ya Elimusingi unaokidhi viwango vya kimataifa.

ii. Kujengea uwezo taasisi za Elimumsingi katika kutengeneza mitaala na kufanya marejeo na uboreshaji wa mitaala kwa kushirikiana na taasisi za nje;

iii. Kuoanisha mitaala ya ndani ili iendane na viwango vya kikanda na kimataifa;

iv. Kuboresha na kuendeleza mitaala ya kujifunzia na kufundishia kwa njia ya masafa;

v. Kuandaa, kuendeleza na kutoa ithibati kwa walimu wenye kukidhi viwango vya kufundisha mitaala ya kimataifa.

vi. Kutoa ithibati kwa taasisi za Elimumsingi kufundisha kwa kutumia mitaala yenye maudhui na viwango vya kimataifa;

vii. Kujenga uwezo wa taasisi rekebu kupokea, kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi;

viii. Kuboresha miundombinu ili kuwezesha utekelezaji wa mitaala kwa njia ya mseto; na

ix. Kushirikisha jamii kuhusu umataifishaji na utekelezaji katika ngazi ya Elimumsingi.

### 4.1.2 Elimu ya juu

#### 4.1.2.1 Malengo

i. Mitaala yenye kuandaa wahitimu wa elimu wenye stadi, ujuzi, maarifa na utaalamu shindani kitaifa, kikanda na kimataifa kuboreshwa;

ii. Wanafunzi toka nje ya nchi kuja kusoma nchini kupitia mitaala iliyoboreshwa kuongezeka; na

iii. Ushirikiano kati ya taasisi za elimu za nje ya nchi na taasisi za ndani katika utengenezaji na utekelezaji wa mitaala kuongezeka.

#### 4.1.2.2 Mikakati

i. Kusimamia utekelezaji wa mitaala ya taifa ya elimu ya juu inayokidhi viwango vya kimataifa.

ii. Kujengea uwezo taasisi za elimu ya juu kutengeneza mitaala na kufanya marejeo na maboresho ya mitaala kwa kushirikiana na taasisi za nje;

iii. Kuoanisha mitaala ya elimu ya juu iendane na viwango vya kikanda na kimataifa ili kuvutia wanafunzi kutoka nje ya nchi;

iv. Kuboresha na kuendeleza mitaala ya kujifunzia na kufundishia kwa njia ya masafa;

v. Kutoa ithibati kwa taasisi za elimu ya juu kufundisha kwa kutumia mitaala yenye maudhui na viwango vya kimataifa;

vi. Kujenga uwezo wa taasisi rekebu kupokea, kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi;

vii. Kuboresha mifumo ya ithibati kati ya taasisi rekebu na mabaraza ya kitaalamu;

viii. Kuboresha miundombinu ili kuwezesha utekelezaji wa mitaala kwa njia mseto; na

ix. Kushirikisha jamii kuhusu umataifishaji na utekelezaji katika ngazi ya elimu ya juu.

## 4.2 Programu za Ushirikiano na Taasisi za Elimu Nje ya Nchi

Uanzishwaji na uendeshaji wa programu za kitaaluma za ushirikiano na taasisi za elimu za nje ni namna mojawapo ya njia ya kubadilishana uzoefu, ujuzi na rasilimali katika ujifunzaji na ufundishaji.

### 4.2.1 Elimu ya juu

#### 4.2.1.1 Malengo

i. Idadi ya wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu kupitia programu za masomo za ushirikiano kuongezeka;

ii. Fursa kwa wahitimu kupata vyeti au shahada zaidi ya moja kwa wakati mmoja kutolewa; na

iii. Wahitimu wanaopata ujuzi na elimu kutoka katika taasisi mbili au zaidi kwa wakati mmoja kuongezeka.

#### 4.2.1.2. Mikakati

i. Kuweka kanuni na miongozo inayowezesha uanzishwaji na uendeshaji wa programu za ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi;

ii. Kuanzisha na kuhuisha mashirikiano na taasisi za elimu ya juu nje ya nchi yanayojikita katika kuendesha programu za ushirikiano;

iii. Kujenga uwezo wa taasisi za elimu ya juu kuanzisha na kuendesha programu za ushirikiano; na

iv. Kushirikisha wadau wote wanaohusika katika kuendesha programu za ushirikiano

## 4.3 Udahili na Uandikishaji wa Wanafunzi Ndani ya Nchi

Udahili/uandikishaji wa wanafunzi katika taasisi za elimu ni hatua ya msingi katika dhana nzima ya umataifishaji. Ili kuweza kufikia malengo ya udahili, mikakati mbalimbali inahitajika kufanyika au kuboreshwa.

### 4.3.1 Elimumsingi

#### 4.3.1.1 Malengo

i. Idadi ya wanafunzi wa kigeni katika taasisi za Elimumsingi nchini kuongezeka;

ii. Taasisi za Elimumsingi kupandishwa hadhi kufikia viwango vya kimataifa;

iii. Mifumo ya uandikishaji wa wanafunzi kwa taasisi za Elimumsingi nchini kuboreshwa;

iv. Utangamano wa mila, desturi na tamaduni za nchi mbalimbali kuimarishwa; na;

v. Mapato ya fedha za kigeni kupitia uandikishaji wa wanafunzi wa kigeni kuongezeka.

#### 4.3.1.2 Mikakati

Mikakati ya utekelezaji kupelekea kutanua wigo wa uandikishaji wa wanafunzi kutoka nje ni pamoja na:

i. Kuwezesha taasisi za Elimumsingi kusimamia uandikishaji wa wanafunzi kutoka nje ya nchi;

ii. Kuboresha Sera, Kanuni na Miongozo ya upatikanaji na usimamizi wa vibali / pasi za masomo kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi;

iii. Kuweka utaratibu unaoruhusu wanafunzi kuandikishwa katika taasisi za Elimumsingi wakati wowote ndani ya mwaka wa masomo;

iv. Kutumia fursa za makubaliano ya kikanda ikiwemo ufadhili na ulinganifu wa ada katika jumuiya za kikanda;

v. Kuboresha ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi;

vi. Kushirikisha Taasisi za Uwakala wa uandikishaji wa wanafunzi wa kimataifa katika taasisi za Elimumsingi;

vii. Kuboresha mifumo ya utangazaji wa programu na huduma zinazotolewa na taasisi za Elimumsingi;

viii. Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili, Kingereza, lugha zingine za kigeni na lugha ya alama;

ix. Kuimarisha utaratibu wa wanafunzi wa kigeni kutembelea vivutio vya utalii Tanzania; na

x. Kuimarisha ushiriki wa maonesho na mashindano ya taasisi za Elimumsingi kimataifa.

#### 4.3.2 Elimu ya juu

##### 4.3.2.1 Malengo

i. Idadi ya wanafunzi wa kigeni katika taasisi za elimu nchini kuongezeka hadi kufikia angalau asilimia tano (5%);

ii. Hadhi za taasisi za elimu ya juu kukua hadi kufikia viwango vya kikanda na kimataifa;

iii. Mifumo ya udahili kwa taasisi za elimu ya juu nchini kuboreshwa;

iv. Utangamano wa mila, desturi na tamaduni za nchi mbalimbali kuimarishwa; na

v. Mapato ya fedha za kigeni kupitia udahili wa wanafunzi wa kigeni kuongezeka.

##### 4.3.2.2 Mikakati

Mikakati ya utekelezaji kupelekea kutanua wigo wa udahili wa wanafunzi kutoka nje ni pamoja na:

i. Kuwezesha ofisi za umataifishaji za taasisi za elimu ya juu, taasisi za uwakala na taasisi rekebu kuratibu udahili wa wanafunzi toka nje ya nchi;

ii. Kujenga uwezo wa taasisi rekebu kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za nje ya nchi;

iii. Kuboresha sera, kanuni na miongozo ya upatikanaji na usimamizi wa vibali/pasi za masomo na kufanya tafiti kwa wanafunzi wa nje;

iv. Kuweka utaratibu unaoruhusu wanafunzi kudahiliwa katika taasisi za elimu ya juu kwa vipindi tofauti ndani ya mwaka wa masomo.

v. Kutumia fursa za makubaliano ya kikanda ikiwemo ufadhili na ulinganifu wa ada katika jumuiya za kikanda;

vi. Kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi katika programu za kimkakati;

vii. Kushirikisha taasisi za uwakala kudahili wanafunzi wa kimataifa katika taasisi za elimu;

viii. Kuboresha mifumo ya utangazaji wa programu na huduma zinazotolewa na taasisi za elimu ya juu;

ix. Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili, Kifaransa, Kichina, Kijerumani, Kiarabu na lugha ya alama ya Tanzania;

x. Kuimarisha utaratibu wa wanafunzi wa kigeni kutembelea vivutio vya utalii Tanzania; na

xi. Kuimarisha ushiriki wa maonyesho na mashindano ya taasisi za elimu ya juu kimataifa.

## 4.4 Udahili na Uandikishaji wa Wanafunzi Kusoma Nje ya Nchi

Moja ya jitihada za umataifishaji wa elimu nchini ni kutafuta fursa za watanzania wenye sifa za kusoma nje ya nchi. Hata hivyo, idadi ya watanzania wanaopata fursa hizo ni ndogo na hivyo kuna umuhimu wa kuandaa mikakati ya kuongeza fursa na idadi ya watanzania kusoma nje ya nchi.

### 4.4.1 Elimumsingi

#### 4.4.1.1 Malengo

i. Idadi ya wanafunzi wa Elimumsingi kusoma nje ya nchi kuongezeka; na

ii. Fursa za ufadhili wa wanafunzi wa Elimumsingi kusoma nje ya nchi kuongezwa.

#### 4.4.1.2 Mikakati

Mikakati ya utekelezaji itakayosaidia kutanua wigo wa uandikishaji wa wanafunzi kwenda nje ni pamoja na:

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa muongozo wa kitaifa wa kuratibu fursa za ufadhili wa wanafunzi wa Elimumsingi;

ii. Kuboresha utangazaji wa fursa za masomo ya Elimumsingi zinazopatikana nchi za nje;

iii. Kushirikiana na taasisi za uwakala kupeleka wanafunzi wa Elimumsingi nchi za nje;

iv. Kuboresha makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi za Elimumsingi za ndani na nje ya nchi;

v. Kuandaa semina na makongamano ili kujenga uelewa wa wananchi kuona fursa za masomo za Elimumsingi nchi za nje;

vi. Kuandaa na kushiriki maonesho na mashindano ya Elimumsingi ya kimataifa; na

vii. Kuboresha na kuunganisha mifumo ya utoaji wa ithibati na utambuzi wa shule nje ya nchi.

### 4.4.2 Elimu ya juu

#### 4.4.2.1 Malengo

i. Idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaosoma nje ya nchi kuongezeka hadi kufikia angalau wanafunzi 5000 kwa mwaka; na

ii. Ufadhili wa elimu ya juu kuwezesha watanzania kusoma nje ya nchi kuongezeka.

#### 4.4.2.2 Mikakati

Mikakati ya utekelezaji itakayosaidia kutanua wigo wa udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu kwenda nje ya nchi ni pamoja na:

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa muongozo wa kitaifa wa kuratibu fursa za ufadhili wa wanafunzi;

ii. Kuboresha utangazaji wa fursa za masomo zinazopatikana nje ya nchi;

iii. Kushirikiana na taasisi za uwakala katika kupeleka wanafunzi nje ya nchi;

iv. Kuboresha ushirikiano kati ya taasisi za ndani na za nje ya nchi;

v. Kuongeza fursa za ufadhilii wa wanafunzi kusoma ndani na nje ya nchi;

vi. Kuandaa semina na makongamano ili kujenga uelewa kwa wananchi kuona fursa za masomo nje ya nchi;

vii. Kuandaa na kushiriki maonesho na mashindano ya elimu ya kimataifa; na

viii. Kuboresha na kuunganisha mifumo ya utoaji wa ithibati na utambuzi wa taasisi za elimu nje ya nchi.

## 4.5 Kuajiri Walimu, Wanataaluma na Wataalamu wengine kutoka Nje ya Nchi

Kuajiri walimu, wanataaluma na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi ni hatua muhimu katika kuingiza ujuzi na uzoefu wa fani mbalimbali. Aidha, hatua hii inawezesha uboreshaji na uandaaji wa wanafunzi na wataalamu nchini. Hata hivyo, idadi ya walimu, wanataaluma na wataalamu wengine wa kigeni walioajiriwa nchini ni ndogo na hivyo kuna haja ya kuandaa mikakati itakayoongeza idadi yao.

### 4.5.1 Elimumsingi

Ili kuongeza ubora na umataifishaji wa Elimumsingi malengo yafatayo yatatekelezwa:-

#### 4.5.1.1 Malengo

i. Idadi ya walimu na wataalamu wengine wenye sifa na wanaotambulika kimataifa kutoka nje ya nchi kuongezeka;

ii. Wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi kuongezeka;

iii. Ujifunzaji na ufundishaji kupitia maarifa na mbinu za kisasa kutoka sehemu mbalimbali za dunia kuimarishwa; na

iv. Utangamano wa mila, desturi chanya katika taasisi za Elimumsingi kukuzwa na kuimarishwa.

#### 4.5.1.2 Mikakati

i. Kuboresha taratibu na miongozo inayosimamia ajira za walimu na wataalamu wengine katika taasisi za Elimumsingi;

ii. Kuboresha Mwongozo wa upatikanaji wa vibali vya kazi kwa walimu na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi

iii. Kuboresha mazingira yanayozovutia walimu na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi; na

iv. Kuandaa programu za mafunzo ya lugha na utamaduni kwa walimu na wataalamu wengine wa kimataifa.

### 4.5.2 Elimu ya Juu

Ili kuongeza ubora na umataifishaji wa elimu ya juu malengo yafuatayo yatatekelezwa:-

#### 4.5.2.1 Malengo

i. Idadi ya wanataaluma na wataalamu wengine wenye sifa zinazotambulika kimataifa kutoka nje ya nchi kuongezeka;

ii. Idadi ya wanafunzi wa nje wanaosoma ndani ya nchi kuongezeka;

iii. Ufundishaji kupitia maarifa na mbinu za kisasa kutoka sehemu mbalimbali za dunia kuimarishwa;

iv. Utangamano wa mila, desturi chanya katika taasisi za elimu ya juu kuimarishwa; na

v. Miradi ya utafiti, mafunzo na ubunifu wa hadhi ya kimataifa kuongezeka.

#### 4.5.2.2 Mikakati

i. Kuboresha na kusimamia kanuni na miongozo ya ajira za wanataaluma na wataalamu wengine katika taasisi za elimu toka nje ya nchi;

ii. Kuboresha taratibu za upatikanaji wa vibali vya kazi kwa wanataaluma na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi;

iii. Kuboresha stahiki za wanataaluma na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi;

iv. Kuboresha miundombinu ya taasisi za elimu ili kuvutia wanataaluma na wataalamu wengine wa kimataifa; na

v. Kuandaa programu za mafunzo ya lugha na utamaduni kwa wanataaluma na wataalamu wengine wa kimataifa ili kuwasaidia kuelewa na kuingiliana vyema na jamii ya wenyeji.

## 4.6 Mabadilishano ya Wanafunzi, Walimu, Wanataaluma na Wataalamu wengine

Mabadilishano ya wanafunzi, walimu, wanataaluma na wataalamu wengine katika taasisi za elimu ni nyenzo muhimu na yenye kuleta tija katika umataifishaji. Programu hizi zinaweza kuwa za muda mfupi au mrefu kulingana na uhitaji na makubaliano ya pande husika. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi, walimu, wanataaluma na wataalamu wengine wanaoshiriki kwenye mabadilishano hairidhishi.

### 4.6.1 Elimumsingi

#### 4.6.1.1 Malengo

i. Kubadilishana ujuzi na uzoefu katika mafunzo, stadi, elimu, ubunifu na teknolojia mbalimbali;

ii. Kutangaza tamaduni zetu na kutambua tamaduni za nchi nyingine; na

iii. Kuongeza fursa za utalii ikiwemo utalii wa elimu nchini.

#### 4.6.1.2 Mikakati

i. Kuboresha miundombinu ya taasisi za Elimumsingi ili kufikia viwango vya kimataifa;

ii. Kuratibu programu za mabadilishano za masomo;

iii. Kuongeza idadi ya walimu na wataalamu wengine wanaoshiriki kufundisha programu za masomo ndani na nje ya nchi;

iv. Kuboresha utaratibu wa kuingia na kutekeleza makubaliano ya mabadilishano ya wanafunzi, walimu na wataalamu wengine;

v. Kuweka utaratibu wa programu za mabadilishano zinazojumuisha utalii wa elimu; na

vi. Kuongeza rasilimali fedha ili kuwezesha programu za mabadilishano ya wanafunzi, walimu na wataalamu wengine.

#### 4.6.2 Elimu ya juu

##### 4.6.2.1 Malengo

i. Mabadilishana ya ujuzi na uzoefu katika masuala ya mafunzo, stadi, elimu, tafiti, ubunifu na teknolojia mbalimbali kuimarishwa;

ii. Matangazo ya tamaduni zetu na utambuzi wa tamaduni za nchi nyingine kuongezeka; na

iii. Fursa za utalii ikiwemo utalii wa elimu nchini kuongezeka.

##### 4.6.2.2 Mikakati

i. Kuboresha miundombinu ya taasisi za elimu ya juu ili kufikia viwango vya kimataifa;

ii. Kuratibu programu za masomo za muda mfupi ili kuwawezesha wanafunzi kutoka nje ya nchi kushiriki programu za mabadilishano;

iii. Kuongeza mabadilishano ya watahini kutoka taasisi za elimu ya juu za ndani na nje ya nchi;

iv. Kuongeza idadi ya wanataaluma na wataalamu wengine wa nje wanaoshiriki kufundisha programu za masomo ndani na nje ya nchi;

v. Kuboresha uratibu na ufanisi wa programu za mabadilishano ya elimu ya juu;

vi. Kuboresha utaratibu wa kuingia na kutekeleza makubaliano ya mabadilishano ya wanafunzi, wanataaluma na wataalamu wengine;

vii. Kuweka utaratibu wa programu za mabadilishano zinazojumuisha utalii wa elimu; na

viii. Kuongeza rasilimali fedha ili kuwezesha programu za mabadilishano ya wataalamu na wanafunzi.

### 4.7 Mashirikiano katika Elimu, Stadi, Utafiti na Ubunifu

Mashirikiano na taasisi za nje katika elimu, stadi, tafiti na ubunifu hupunguza au kuondoa changamoto mbalimbali katika jamii, viwanda na uchumi. Aidha, mashirikano hayo yanaweza kuchochea ukuaji wa umataifishaji katika taasisi za elimu. Hata hivyo, idadi na manufaa ya mashirikiano bado hayaridhishi. Ni muhimu kuweka malengo na mikakati ili kufikia mashirikiano hayo.

#### 4.7.1 Elimumsingi

##### 4.7.1.1 Malengo

i. Ujuzi, stadi na uzoefu wa kimataifa kwa wanafunzi na walimu katika Elimumsingi kuongezeka; na

ii. Fursa za upatikanaji wa rasilimali fedha na watu ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji kuongezeka.

##### 4.7.1.2 Mikakati

i. Kuanzisha na kutekeleza mashirikiano yanayolenga kuboresha ujifunzaji na ufundishaji;

ii. Kujenga uwezo wa walimu na wataalamu wengine katika kuanzisha na kutekeleza mashirikiano;

iii. Kutambua na kuendeleza vipaji na ubunifu kupitia mashirikiano ya kimataifa; na

iv. Kuandaa na kushiriki kwa pamoja makongomano na mashindano ya elimu, ustadi na ubunifu kimataifa.

#### 4.7.2 Elimu ya juu

##### 4.7.2.1 Malengo

i. Ujuzi na stadi maalumu kutokana na mashirikiano yanayotekelezwa kupitia miradi ya elimu, stadi, utafiti na ubunifu kuongezeka; na

ii. Fursa za upatikanaji wa miundombinu na vifaa vya kisasa kwa ajili ya mafunzo na tafiti kuongezeka.

##### 4.7.2.2 Mikakati

i. Kuanzisha na kutekeleza makubaliano ya ushirikiano kwenye maeneo ya ubobezi na umahiri;

ii. Kuboresha uwezo wa kuandika miradi ya kimkakati ili kuongeza ubobezi kwenye mafunzo, utafiti na ubunifu:

iii. Kuboresha utaratibu na miongozo ya kutoa motisha kwa watafiti na wabunifu kuweza kubiasharisha na kuchapisha kwenye majarida yenye hadhi ya kimataifa;

iv. Kujenga umahiri kwenye maeneo mahususi ya utafiti na ubunifu;

v. Kuwezesha watafiti na wabunifu wachanga kupata uzoefu wa stadi za tafiti na bunifu za viwango vya kimataifa;

vi. Kuchapisha matokeo ya kitafiti na kibunifu kwa pamoja katika majarida ya kimataifa;

vii. Kuandaa na kushiriki kwa pamoja makongomano ya kielimu, kiustadi, kitafiti na kibunifu ya kimataifa;

viii. Kujenga uwezo wa ubiasharishaji wa matokeo ya stadi, tafiti na bunifu kupitia vituo atamizi; na

ix. Kuwa na utaratibu wa kumiliki haki miliki za matokeo ya stadi, tafiti na bunifu kwa pamoja.

## 4.8 Taasisi za Elimu Nje ya Nchi

Ili kukuza umataifishaji, ni muhimu kwa taasisi za elimu kujipanua na kuanzisha programu za masomo nje ya nchi kupitia kampasi/shule/vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti. Uanzishwaji wa programu hizo unatoa fursa kwa taasisi za elimu nchini kuongeza udahili au uandikishaji wa wanafunzi wa kimataifa na kuinua hadhi ya taasisi husika. Hata hivyo, taasisi nyingi hazijaweza kutumia fursa hii ya kuanzisha programu za masomo nje ya nchi.

### 4.8.1 Elimumsingi

#### 4.8.1.1 Malengo

i. Viwango vya umataifishaji kupitia shule nje ya nchi kuongezeka;

ii. Uzoefu na umahiri wa wanafunzi kupitia programu zinazotolewa na shule kuongezeka; na

iii. Mapato ya shule kutokana na makusanyo ya ada kutokana na ongezeko la wanafunzi wa kigeni katika shule za nje ya nchi kuongezeka.

#### 4.8.1.2 Mikakati

i. Kuratibu uanzishwaji wa matawi ya shule au shule nje ya nchi; na

ii. Kuweka miongozo kwa walimu na wataalamu wengine nchini kwenda kufundisha na kufanya kazi katika shule husika nje ya nchi.

### 4.8.2 Elimu ya juu

#### 4.8.2.1 Malengo

i. Viwango vya umataifishaji wa elimu ya juu kupitia kampasi/shule/vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi kuongezeka;

ii. Uzoefu na umahiri wa wanafunzi wa elimu ya juu kupitia programu zinazotolewa na kampasi/shule/vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi kuimarishwa; na

iii. Mapato ya taasisi za elimu ya juu za ndani kutokana na makusanyo ya ada kutoka kwa wanafunzi wa kigeni kuongezeka.

#### 4.8.2.2 Mikakati

i. Kuratibu uanzishaji wa taasisi za elimu (Chuo/kampasi/vituo vya mafunzo na utafiti) nje ya nchi;

ii. Kubainisha sekta za kipaumbele za kitaalamu zinazoweza kuvutia wanafunzi katika nchi husika;

iii. Kuanzisha kampasi/shule/vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi kupitia makubaliano ya ushirikiano na taasisi za elimu za nje ya nchi; na

iv. Kuweka utaratibu kwa wanataaluma na wataalamu wengine nchini kufundisha, kufanya utafiti, ubunifu na kufanya kazi katika kampasi/shule/vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi.

## 4.9 Taasisi za Elimu za Nje ndani ya Nchi

Ili kukuza umataifishaji ndani ya nchi, taasisi za elimu za nje ya nchi zina fursa ya kufungua kampasi/shule/vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti ndani ya nchi. Utaratibu huu utapanua wigo na kutoa fursa kwa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi kusoma katika taasisi za elimu ndani ya nchi.

### 4.9.1 Elimumsingi

#### 4.9.1.1 Malengo

i. Viwango vya umataifishaji kupitia shule zilizoanzishwa ndani ya nchi na taasisi za elimu kutoka nje ya nchi kuongezeka;

ii. Teknolojia na umahiri wa ujifunzaji na ufundishajii katika taasisi za Elimumsingi za nje na ndani ya nchi kuongezeka;

iii. Idadi ya uandikishaji wa wanafunzi wa Elimumsingi ndani na nje ya nchi kuongezeka;

iv. Fursa kwa wanafunzi wa Elimumsingi kujifunza tamaduni za nchi mbalimbali ili kuleta utangamano kutolewa; na

v. Mapato ya fedha za kigeni kupitia uandikishaji wa wanafunzi kutoka nje ya nchi kuongezeka.

#### 4.9.1.2 Mikakati

i. Kuboresha miongozo ya kuanzisha na kusimamia shule kutoka nje ya nchi; na

ii. Kuweka utaratibu kwa walimu na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi kufanya kazi ndani ya nchi.

### 4.9.2 Elimu ya juu

#### 4.9.2.1 Malengo

i. Viwango vya umataifishaji kupitia kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti vya taasisi za elimu ya juu kutoka nje ya nchi kuongezeka;

ii. Matumizi ya teknolojia na umahiri unaoletwa na taasisi za elimu za nje ndani ya nchi kuongezeka;

iii. Udahili wa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi wa elimu ya juu kuongezeka;

iv. Fursa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kujifunza tamaduni za nchi mbalimbali ili kuleta utangamano wa kimataifa kuongezeka; na

v. Mapato ya fedha za kigeni kupitia udahili wa wanafunzi kutoka nje ya nchi kuongezeka.

#### 4.9.2.2 Mikakati

i. Kuboresha miongozo na usimamizi wa kuanzisha kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti za taasisi za elimu kutoka nje ya nchi;

ii. Kubainisha na kuendesha programu za kipaumbele za ufundi, stadi za kazi, kitaaluma, utafiti na ubunifu zinazohitajika ndani ya nchi;

iii. Taasisi za elimu za nje ya nchi kuanzisha kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti za ndani kupitia makubaliano ya ushirikiano na taasisi za elimu za ndani ya nchi;

iv. Kuweka utaratibu kwa wanataaluma na wataalamu wengine nchini kuweza kufundisha na kufanya kazi katika kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti ndani na nje ya nchi; na

v. Kushirikisha wizara za kisekta kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti za ndani kutoka taasisi za elimu nje ya nchi.

## 4.10 Lugha ya Kiswahili

Kwa kuwa Tanzania ni chimbuko la lugha ya Kiswahili na matumizi ya lugha ya Kiswahili yanaongezeka kwa kasi barani Afrika na duniani, kuna fursa kubwa kwa Tanzania

kufundisha, kufanya utafiti na kujenga ubobezi wa lugha ya Kiswahili duniani. Aidha, taasisi za elimu nchini zina fursa ya kufundisha lugha za kigeni sambamba na lugha ya Kiswahili ili kuimarisha dhana ya umataifishaji.

#### 4.10.1 Malengo

i. Ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kupitia programu za mafunzo na utafiti kuimarishwa;

ii. Matumizi ya kitaaluma ya lugha ya Kiswahili duniani kuhamasishwa; na

iii. Wataalamu wa lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni wenye uwezo wa kuajiriwa kitaifa, kikanda na kimataifa kuongezeka.

#### 4.10.2 Mikakati

i. Kufundisha lugha ya Kiswahili kitaifa, kikanda na kimataifa katika ngazi zote za elimu;

ii. Kuboresha mitaala, mafunzo na utafiti wa lugha ya Kiswahili;

iii. Kuifanya lugha ya Kiswahili kama somo kwenye programu za kimkakati zenye ufadhili unaotolewa na serikali au taasisi za elimu ndani ya nchi;

iv. Kuandaa na kushiriki mashindano na makongamano ya kitaaluma ya lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani;

v. Kuanzisha mashirikiano na taasisi za elimu nje ya nchi zinazofundisha lugha za kigeni;

vi. Kuanzisha programu za mabadilishano ya wanataaluma na wanafunzi wa Kiswahili na lugha za kigeni;

vii. Kuweka miundombinu inayohitajika katika kujifunzia na kufundishia lugha; na

viii. Kuweka kanuni na miongozo inayowezesha ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na za kigeni nchini.

### 4.11 Matumizi ya Balozi za Ndani na Nje ya Nchi

Balozi ni taasisi muhimu katika kufanikisha malengo ya umataifishaji wa elimu. Hii inatokana na dhamana zilizonazo katika kuwakilisha nchi husika.

#### 4.11.1 Malengo

i. Fursa za mashirikiano, ufadhili wa masomo na mabadilishano ya walimu, wakufunzi, wanataaluma na wataalamu wengine,kuongezeka; na

ii. Fursa za mafunzo ya lugha mbalimbali kupitia mahusiano kati ya Balozi na taasisi za elimu ndani na nje ya nchi kuongezeka.

#### 4.11.2 Mikakati

i. Kuimarisha ofisi za uambata wa elimu katika Balozi nje ya nchi;

ii. Kuboresha upatikanaji wa fursa za ujifunzaji wa lugha za kigeni nchini;

iii. Kuimarisha mahusiano kati ya taasisi za elimu ndani na nje ya nchi ili kuongeza fursa za masomo ya lugha mbalimbali;

iv. Kuimarisha utaratibu wa ushirikiano na taasisi za uwakala ili kuongeza ufanisi katika uandikishaji na udahili wa wanafunzi ndani na nje ya nchi; na

v. Kuboresha mifumo ya ufuatiliaji mienendo na maendeleo ya wanafunzi ya kitaaluma na kijamii wanaosoma nje ya nchi.

### 4.12 Taasisi za Uwakala wa Elimu Ndani ya Nchi

Serikali au taasisi za elimu zinafursa kutumia taasisi za uwakala wa elimu zilizosajiliwa ili kuongeza kiwango cha uandikishaji, udahili, mashirikiano na fursa za umataifishaji kati ya taasisi za elimu ndani na nje ya nchi. Hata hivyo kuna haja ya kuboresha ushirikishwaji wa taasisi za uwakala katika kukuza na kuongeza umataifishaji wa elimu nchini.

#### 4.12.1 Malengo

i. Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika taasisi za elimu ndani na nje ya nchi kupitia Wakala wa Elimu kuongezeka;

ii. Fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi kuongezeka; na

iii. Matumizi ya fursa zinazotokana na mashirikiano kati ya taasisi za elimu ndani na nje ya nchi kuimarishwa.

#### 4.12.2 Mikakati

i. Kuboresha miongozo na majukumu ya wakala wa uandikishaji na udahili wa wanafunzi wa elimu ndani na nje ya nchi;

ii. Kuimarisha makubaliano ya ushirikiano kati ya wakala, wizara na taasisi za elimu;

iii. Kuboresha mahusiano kati ya wakala na balozi za ndani na nje ya nchi;

iv. Kujenga uwezo wa mawakala kujiendesha kulingana na sheria, kanuni na taratibu za udahili wa wanafunzi;

v. Kutumia mawakala kubaini programu na fursa zitakazo saidia kuendeleza vipaumbele vya nchi katika kudahili wanafunzi ndani na nje ya nchi; na

vi. Kuziwezesha taasisi za uwakala kufuatilia mienendo na maendeleo ya wanafunzi wanaosoma nje ya nchi.

## 4.13 Udahili wa Wanafunzi Kutoka Nchi Zenye Majanga

Tanzania imekuwa na historia ya kupokea wanafunzi kutoka nchi zinazokabiliwa na majanga mbalimbali. Wanafunzi hao huhitaji huduma mbalimbali ikiwemo huduma za elimu. Umataifishaji wa elimu unaweza kutoa fursa kwa wanafunzi hawa kukamilisha malengo yao ya elimu.

### 4.13.1 Malengo

i. Fursa kwa wanafunzi wanaotoka katika nchi zilizoathirika na majanga mbalimbali kuimarishwa; na

ii. Diplomasia kati ya nchi ya Tanzania na nchi zilizoathirika na majanga kuimarishwa.

### 4.13.2 Mikakati

i. Kuboresha miongozo na taratibu za kupokea, kuandikisha na kudahili wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga;

ii. Kuimarisha mifumo ya utambuzi wa sifa za elimu, uandikishaji, udahili na usimamizi wa wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga;

iii. Kuingia makubaliano na taasisi zinazotoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga;na

iv. Kuimarisha ushirikiano na Balozi pamoja na taasisi za kimataifa ili kuweka utaratibu wa kusimamia na kutatua changamoto za wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga.

# SURA YA TANO

## 5. MPANGILIO WA KITAASISI NA MAJUKUMU

Ili kufanikisha Mkakati wa umataifishaji wa elimu, ushiriki wa wadau mbalimbali kwa kuzingatia majukumu yao unahitajika. Wadau hao ni pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Taasisi za elimu, Taasisi Rekebu, Balozi za Tanzania na Mawakala wa elimu. Hivyo, sura hii inaeleza mpangilio wa majukumu na uwajibikaji wa taasisi mbalimbali za umma na zile za binafsi.

### 5.1 Majukumu ya Serikali

Pamoja na usimamizi wa jumla wa utekelezaji wa Mkakati huu, Serikali kupitia WyEST, itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuendelea kuboresha Sera ya Elimu kuendana na mahitaji ya umataifishaji;

ii. Kuweka mfumo wa utekelezaji wa Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu nchini;

iii. Kusimamia utekelezaji wa muundo wa ithibati na udhibiti wa ubora katika elimu;

iv. Kuwezesha taasisi za elimu kutekeleza majukumu ya umataifishaji wa elimu kulingana na Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu nchini;

v. Kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Mkakati wa Umataifishaji wa elimu nchini;

vi. Kuanzisha dawati litakaloratibu shughuli za umataifishaji katika ngazi ya taifa;

vii. Kusomesha walimu, wakufunzi, wanataaluma na wataalamu wengine kwenye vyuo bora vya kimataifa nje ya nchi;

viii. Kutenga fedha za ufadhili wa wanafunzi kusoma ndani na nje ya nchi;

ix. Kushirikisha taasisi zinazotegemeana katika utekelezaji wa Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu nchini;

x. Kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa umataifishaji wa elimu;

xi. Kuingia na kusimamia mashirikiano ya kimkakati na nchi za nje katika jitihada za kuimarisha umataifishaji wa elimu;

xii. Kuandaa mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo nje ya nchi;

xiii. Kuweka mfumo wa kutangaza fursa za masomo nje ya nchi;

xiv. Kuandaa mwongozo wa kuongeza fursa za ajira za elimu nje ya nchi; na

xv. Kusimamia uoanishaji wa vigezo vya ithibati kati ya taasisi rekebu na mabaraza ya kitaalamu ya ndani na nje ya nchi.

## 5.2 Majukumu ya Taasisi za Elimu

Katika kutekeleza Mkakati wa umataifishaji wa elimu, taasisi za elimu zitatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuanzisha dawati, vitengo au kurugenzi za umataifishaji katika taasisi;

ii. Kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na miongozo ya umataifishaji wa elimu katika taasisi;

iii. Kuandaa na kutekeleza mipango kazi ya utekelezaji wa sera, mikakati na miongozo ya umataifishaji wa elimu katika taasisi;

iv. Kuhakikisha uwepo wa mitaala yenye sifa za kimataifa katika taasisi za elimu nchini;

v. Kuhakikisha programu na taasisi zinajitangaza ndani na nje ya nchi;

vi. Kutenga rasilimali za utekelezaji wa sera, mikakati na miongozo ya umataifishaji wa elimu katika taasisi;

vii. Kutoa huduma za usaidizi kwa walimu, wakufunzi, wanataaluma, wataalamu wengine, na wanafunzi wanaoshiriki katika programu za umataifishaji;

viii. Kuingia na kutekeleza makubaliano ya mashirikiano ya umataifishaji wa elimu na taasisi za elimu za nje ya nchi;

ix. Kuweka mfumo wa uwasilishaji wa taarifa za umataifishaji wa elimu katika taasisi za elimu katika ngazi mbalimbali;

x. Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuwezesha utekelezaji wa mitaala kwa njia ya mseto; na

xi. Kuhakikisha taasisi za elimu zina miundombinu wezeshi kufikia viwango vya kimataifa.

## 5.3 Majukumu ya Taasisi Rekebu

Katika kutekeleza Mkakati wa umataifishaji wa elimu, Taasisi rekebu zitatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa mitaala yenye viwango vya kimataifa nchini;

ii. Kujengea uwezo taasisi za elimu kufanya marejeo na kutengeneza mitaala yenye kuzingatia umataifishaji;

iii. Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuwezesha utekelezaji wa huduma zinazotolewa na taasisi za ithibati kwa taasisi za ndani na nje ya nchi;

iv. Kujenga uwezo wa taasisi za elimu ya juu wa kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za nje ya nchi katika udahili wa wanafunzi;

v. Kuboresha mfumo wa ithibati ya utambuzi wa vyuo vya nje ya nchi;

vi. Kuweka utaratibu na kuboresha miongozo ya kuanzisha taasisi za elimu nje ya nchi; na

vii. Kusajili taasisi za uwakala kwa kuzingatia vigezo.

### 5.4 Majukumu ya Balozi

Katika kutekeleza Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu, Balozi zitatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kutafuta fursa za kielimu nje ya nchi;

ii. Kuunganisha taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi katika umataifishaji;

iii. Kutangaza programu za masomo na taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi;

iv. Kuwezesha mashirikiano kati ya taasisi za uwakala wa elimu na taasisi za elimu ndani na nje ya nchi;

v. Kutoa huduma za usaidizi kwa wanafunzi, walimu, wakufunzi, wanataaluma, na wataalamu wengine wanaoshiriki katika programu za umataifishaji nje ya nchi;

vi. Kubaini wataalamu na taasisi mahiri na bobezi katika maeneo ya elimu na utafiti kutoka nchi za nje; na

vii. Kusaidia uratibu na uandaaji wa maonesho na mashindano ya elimu kimataifa.

### 5.5 Majukumu ya Taasisi za Uwakala

Katika kutekeleza Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu, taasisi za uwakala wa elimu zitatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kushiriki kuongeza uandikishaji na udahili wa wanafunzi wanaosoma katika taasisi za ndani na nje ya nchi;

ii. Kuwezesha matumizi ya fursa zinazotokana na mashirikiano kati ya taasisi za elimu ndani na nje ya nchi;

iii. Kushiriki katika kubaini programu na fursa zitakazo saidia kuendeleza vipaumbele vya nchi katika kudahili wanafunzi ndani na nje ya nchi;

iv. Kutangaza fursa za masomo zinazopatikana ndani na nje ya nchi;

v. Kubaini taasisi mahiri na bobezi katika maeneo ya elimu na utafiti kutoka nje ya nje;

vi. Kujenga uelewa kwa wananchi katika kuona fursa za masomo nje ya nchi; na

vii. Kushiriki kuandaa mashindano na maonesho ya elimu ya kimataifa ndani na nje ya nchi.

# SURA YA SITA

## 6. UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ili kufanikisha utekelezaji wa Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu, ni muhimu kuweka mfumo na utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini. Lengo la ufuatiliaji na tathmini ni kuhakikisha kuwa malengo ya mkakati yaliyokusudiwa yanafikiwa na changamoto za utekelezaji zinajulikana na kutatuliwa kwa wakati.

Ufuatiliaji na Tathmini utafanyika katika ngazi mbalimbali za utekelezaji wa mkakati kila mwaka kulingana na viashiria kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu (**Jedwali Na. 1 )**.

Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini zitatolewa kwa kila ngazi inayofanya Ufuatiliaji na kuiwasilisha ngazi ya juu kwa kutumia mfumo uliopo na kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizopo. Taarifa ya ufuatiliaji na tathmini itatumika katika kuijulisha wizara na wadau husika kwa ajili ya maboresho ya mkakati.

### JEDWALI LA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MKAKATI WA UMATAIFISHAJI KATIKA ELIMU

### JEDWALI NA. 1 (a): ELIMUMSINGI

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| **UMATAIFISHAJI WA MITAALA** | | | | |
| 1 | Kusimamia utekelezaji wa mitaala ya taifa ya Elimumsingi unaokidhi viwango vya kimataifa. | Idadi ya mitaala iliyosimamiwa na kutekelezwa. | 2025 - 2029 | WyEST, TET |
| 2 | Kujengea uwezo taasisi za Elimumsingi katika kutengeneza mitaala na kufanya marejeo na uboreshaji wa mitaala yenye kuzingatia dhana, maudhui na mafunzo kwa njia ya vitendo katika viwango vya kimataifa. | Idadi ya taasisi zilizojengewa uwezo.<br>Idadi ya mafunzo ya kujengea uwezo taasisi<br>Idadi ya mitaala iliyoboreshwa. | 2025- 2026 | WyEST, TET |
| 3 | Kuoanisha mitaala ya ndani ili iendane na viwango vya kikanda na kimataifa. | Idadi ya mitaala iliyooanishwa. | 2025-2026 | TET |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Kuboresha na kuendeleza mitaala ya kujifunzia na kufundishia kwa njia za masafa. | Idadi ya mitaala iliyo boreshwa na kuendelezwa. | 2025 - 2027 | TET |
| 5 | Kuandaa, kuendeleza na kutoa ithibati kwa walimu wenye kukidhi viwango vya kufundisha mtaala wa kimataifa. | Idadi ya walimu waliopewa ithibati. | 2025-2029 | NECTA na<br>Taasisi za Elimumsingi |
| 6 | Kutoa ithibati kwa taasisi za Elimumsingi kufundisha kwa kutumia mitaala yenye maudhui na viwango vya kimataifa. | Idadi ya taasisi za elimumsingi zilizopewa ithibati. | 2025-2029 | NECTA,<br>Taasisi za Elimumsingi. |
| 7 | Kujenga uwezo wa taasisi rekebu kupokea, kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi. | Idadi ya watumishi waliojengewa uwezo.<br>Idadi ya vyeti vilivyofanyiwa ithibati. | 2025-2029 | WyEST,<br>Taasisi Rekebu |
| 8 | Kuboresha miundombinu ili kuwezesha utekelezaji wa mitaala kwa njia ya mseto. | Idadi ya miundombinu iliyoboreshwa.<br>Taarifa ya utekelezaji. | 2025 - 2029 | Taasisi za Elimumsingi |
| 9 | Kushirikisha jamii kuhusu umataifishaji na utekelezaji katika ngazi ya Elimumsingi. | Idadi ya mikutano;<br>idadi ya watu walioshiriki; na idadi ya matangazo. | 2025-2029 | WyEST;<br>Taasisi za elimu ya juu;<br>Taasisi za Uwakala |
| **PROGRAMU ZA USHIRIKIANO NA TAASISI ZA ELIMU NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuweka kanuni na miongozo inayowezesha uanzishwaji na uendeshwaji wa programu za ushirikiano kati ya taasisi za ndani na nje. | Idadi ya Kanuni na miongozo mipya.<br>Idadi ya Kanuni na Miongozo iliyoboreshwa. | 2025 | WyEST, Taasisi za Elimumsingi |
| 2 | Kujengea uwezo wa taasisi kuanzisha na kuendesha programu za ushirikiano. | Idadi ya Programu za mafunzo ya ushirikiano zilizoanzishwa. | 2025 -2029 | WyEST, Taasisi za Elimumsingi |
| 3 | Kuanzisha na kuhuisha mashirikiano na taasisi za nje yanayojikita katika kuanzisha programu za aina hii. | Idadi ya taasisi zinazoendesha programu za ushirikiano. | 2025-2029 | Taasisi za Elimumsingi |
| 4 | Kushirikisha wadau wote wanaohusika katika kuendesha programu za ushirikiano. | Idadi ya wadau walioshiriki. | 2025 - 2029 | Taasisi za Elimumsingi |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| **UDAHILI NA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI NDANI YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuwezesha taasisi za Elimumsingi kusimamia uandikishaji wa wanafunzi kutoka nje ya nchi. | Idadi ya taasisi za Elimumsingi zilizowezeshwa.<br>Idadi ya wanafunzi walioandikishwa. | 2025-2026 | WyEST,<br>Taasisi za Elimumsingi |
| 2 | Kuboresha sera, kanuni na miongozo ya upatikanaji na usimamizi wa vibali/pasi za masomo kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi. | Idadi ya sera, kanuni na miongozo iliyoboreshwa. | 2025 - 2026 | WyEST (NECTA, Ofisi ya Kamishna wa Elimu) ,<br>Wizara ya Mambo ya Ndani,<br>Taasisi za Elimumsingi |
| 3 | Kuweka utaratibu unaoruhusu wanafunzi kuandikishwa katika taasisi za Elimumsingi wakati wowote ndani ya mwaka wa masomo. | Idadi ya vipindi vya udahili kwa mwaka. | 2025-2026 | WyEST,<br>Taasisi za elimumsingi |
| 4 | Kutumia fursa za makubaliano ya kikanda ikiwemo ufadhili na ulinganifu wa ada katika jumuiya za kikanda. | Idadi ya fursa zilizopatikana kutokana na ufadhili na ulinganifu wa ada katika jumuiya za kikanda. | 2025-2026 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, WyEST, Taasisi za Elimumsingi |
| 5 | Kuboresha ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi. | Idadi ya programu zilizofadhiliwa.<br>Idadi ya wanafunzi waliofadhiliwa.<br>Idadi ya taasisi zinazotoa ufadhili. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimumsingi,<br>Mawakala wa Elimu,<br>Balozi,<br>Sekta binafsi,<br>Mashirika ya dini,<br>Watu binafsi |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Kushirikisha taasisi za uwakala wa uandikishaji wa wanafunzi wa kimataifa katika taasisi za Elimumsingi. | Idadi ya mawakala walioshirikishwa.<br><br>Idadi ya wanafunzi walioandikishwa na taasisi za uwakala. | 2025-2029 | WyEST,<br><br>Taasisi za Elimumsingi,<br><br>Mawakala wa elimu. |
| 7 | Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili, Kingereza, lugha zingine za kigeni na lugha ya alama. | Idadi ya programu za lugha mbalimbali zilizoanzishwa.<br><br>Idadi ya taasisi za Elimumsingi zinazoendesha programu za lugha.<br><br>Idadi ya wataalamu wa lugha mbalimbali.<br><br>Idadi ya wanafunzi walioandikishwa kwenye programu za Lugha mbalimbali. | 2025-2029 | WyEST,<br><br>OR-TAMISEMI,<br><br>TET, |
| 8 | Kuimarisha utaratibu wa wanafunzi wa kigeni kutembelea vivutio vya utalii Tanzania. | Idadi ya wanafunzi wa kigeni waliotembelea vivutio vya utalii. | 2025-2029 | Tasisi za Elimumsingi nchini,<br><br>Mamlaka zinazosimamia vivutio vya utalii. |
| 9 | Kuimarisha ushiriki wa maonesho na mashindano ya taasisi za Elimumsingi kimataifa. | Idadi ya taasisi za elimu zilizoshiriki maonesho na mashindano ya kimataifa.<br><br>Idadi ya maenesho ya kimataifa yaliyoendeshwa.<br><br>Idadi ya Wanafunzi walioshiriki maonesho na mashindano ya kimataifa. | 2025-2029 | WyEST,<br><br>OR-TAMISEMI,<br><br>Taasisi za Elimumsingi,<br><br>Mawakala wa elimu,<br><br>Balozi za Tanzania nje ya nchi. |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| **UDAHILI NA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI KUSOMA NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa kitaifa wa kuratibu fursa za ufadhili wa wanafunzi wa Elimumsingi. | Mwongozo kukamilika. | Oktoba, 2025 | WyEST |
| | | Taarifa ya usimamizi na utekelezaji wa mwongozo. | 2025-2029 | |
| 2 | Kuboresha utangazaji wa fursa za masomo ya Elimumsingi zinazopatikana nchi za nje. | Idadi ya njia za utangazaji zilizotumika.<br>Idadi za fursa zilizotangazwa<br>na zinazopatikana.<br>Idadi ya wanafunzi wanaoshiriki. kwenye fursa | 2025-2029 | WyEST, Balozi za ndani na nje, Taasisi za Uwakala, Taasisi za Elimu |
| 3 | Kushirikiana na taasisi za uwakala kupeleka wanafunzi wa Elimumsingi nchi za nje. | Idadi ya Hati za makubaliano kati ya taasisi za uwakala na taasisi za elimu.<br>Idadi ya wanafunzi walioandikishwa kupitia taasisi za uwakala. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu (TCU, NACTVET), Taasisi za Elimu, Taasisi za Uwakala |
| 4 | Kuboresha ushirikiano kati ya taasisi za Elimumsingi za ndani na nje ya nchi. | Idadi ya hati za makubaliano zilizosainiwa.<br>Idadi ya wanafunzi wanaofaidika na makubaliano ya mashirikiano. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu, Taasisi za Uwakala |
| 5 | Kuandaa semina na makongamano ili kujenga uelewa kwa wananchi kuona fursa za masomo nchi za nje na kuweza kupeleka watoto wao kusoma nje ya nchi. | Idadi ya semina na makongamano yaliyoandaliwa.<br>Idadi ya wanafunzi waliandikishwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu, Taasisi za Uwakala |
| 6 | Kuboresha na kuunganisha mifumo ya utoaji wa ithibati na utambuzi wa shule nje ya nchi. | Idadi ya mifumo iliyounganishwa. | Desemba, 2025 | WyEST |
| | | Idadi ya ithibati zilizotolewa. | 2025-2029 | |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| **KUAJIRI WALIMU, WANATAALUMA NA WATAALAMU WENGINE KUTOKA NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuboresha taratibu na miongozo inayosimamia ajira za walimu na wataalamu wengine katika taasisi za Elimumsingi. | Idadi ya Miongozo iliyoboreshwa. | 2025-2026 | WyEST |
| | | Idadi ya taasisi zilizoajiri wataalamu wa nje.<br>Idadi ya wataalamu wa nje walioajiriwa. | 2025-2029 | WyEST,<br>Taasisi za Elimu |
| 2 | Kuboresha Mwongozo wa upatikanaji wa vibali vya kazi kwa walimu na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi. | Mwongozo ulioboreshwa. | 2025-2026 | WyEST |
| | | Idadi ya taasisi zilizoajiri walimu na wataalamu wa nje.<br>Idadi ya walimu na wataalamu wa nje walioajiriwa. | 2025-2029 | WyEST;<br>Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na wenye ulemavu; Taasisi za Elimumsingi |
| 3 | Kuboresha mazingira yanayowavutia walimu na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi. | Mwongozo ulioboreshwa. | 2025-2026 | WyEST; |
| | | Idadi ya walimu na wataalamu kutoka nje ya nchi walionufaika.<br>Idadi ya miundombinu iliyoboreshwa. | 2025-2029 | Taasisi za Elimumsingi |
| 4 | Kuandaa programu za mafunzo ya lugha na utamaduni kwa walimu na wataalamu wengine wa kimataifa. | Idadi ya programu za mafunzo ya lugha na tamaduni zilizoandaliwa.<br>Idadi ya wanufaika wa programu. | 2025-2029 | Taasisi za Elimumsingi |
| **MABADILISHANO YA WANAFUNZI, WALIMU, WANATAALUMA NA WATAALAMU WENGINE** | | | | |
| 1 | Kuratibu programu za mabadilishano za masomo. | Idadi ya programu za masomo zilizoratibiwa.<br>Idadi ya taasisi za elimu zinazoshiriki.<br>Idadi ya Wanafunzi, walimu na wataalamu walioshiriki.<br>Idadi ya Programu zilizojumuisha utalii wa elimu. | 2025-2029 | WyEST;<br>OR-TAMISEMI,<br>TET,<br>Taasisi za Elimumsingi |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Kuongeza idadi ya walimu na wataalamu wengine wanaoshiriki kufundisha programu za masomo ndani na nje ya nchi. | Idadi ya walimu na wataalamu. | 2025-2029 | WyEST;<br>OR-TAMISEMI,<br>Taasisi za Elimu |
| 3 | Kuongeza rasilimali fedha ili kuwezesha programu za mabadilishano ya wanafunzi, walimu na wataalamu wengine. | Fedha zilizotengwa kwa ajii ya mabadilishano.<br>Idadi ya Maandiko ya kutafuta fedha za Ufadhili. | 2025-2026 | WyEST, Taasisi za Elimu |
| **MASHIRIKIANO KATIKA ELIMU, STADI, UTAFITI NA UBUNIFU** | | | | |
| 1 | Kuanzisha na kutekeleza mashirikiano yanayolenga kuboresha ujifunzaji na ufundishaji. | Idadi ya mashirikiano yaliyoanzishwa. | 2025-2029 | WyEST;<br>OR-TAMISEMI,<br>Taasisi za elimu |
| 2 | Kujenga uwezo wa walimu na wataalamu wengine katika kuanzisha na kutekeleza mashirikiano. | Idadi ya walimu na wataalamu wengine waliojengewa uwezo.<br>Idadi ya taasisi zilizojengewa uwezo. | 2025-2027 | WyEST;<br>OR-TAMISEMI,<br>Taasisi za elimu, |
| 3 | Kutambua na kuendeleza vipaji na ubunifu kupitia mashirikiano ya kimataifa. | Idadi ya wanafunzi wenye vipaji.<br>Idadi ya program atamizi. | 2025-2026 | WyEST;<br>OR-TAMISEMI,<br>TET,<br>Taasisi za elimu, COSTECH |
| **TAASISI ZA ELIMU NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuratibu uanzishwaji wa matawi ya shule au shule nje ya nchi. | Idadi ya shule au matawi yaliyoanzishwa nje ya nchi.<br>Idadi ya programu zilizotangazwa. | 2027-2029 | WyEST;<br>OR-TAMISEMI,<br>NECTA,<br>TET,<br>Taasisi za Elimu<br>Balozi za<br>Tanzania nje ya nchi |

| SN | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Kuweka utaratibu kwa walimu na wataalamu wengine nchini kwenda kufundisha na kufanya kazi katika shule husika nje ya nchi. | Idadi ya walimu na wataalamu wa nchini waliopata fursa kufundisha na kufanya kazi nje ya nchi. | 2027-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu |
| **TAASISI ZA ELIMU ZA NJE NDANI YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuboresha miongozo na usimamizi wa kuanzisha shule kutoka nje ya nchi. | Idadi ya matawi/shule za kimataifa zilizoanzishwa.<br><br>Idadi ya wizara za kisekta na taasisi zilizoshirikishwa. | 2026-2029 | WyEST,<br>Wizara za kisekta; Taasisi za elimu |
| 2 | Kuweka utaratibu kwa walimu na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi kufanya kazi ndani ya nchi. | Idadi ya walimu na wataalamu kutoka nje ya nchi wanaofanya kazi ndani ya nchi. | 2025 | WyEST, Taasisi rekebu, OWM-KVAU Taasisi za Elimu |

## JEDWALI NA. 1 (b): ELIMU YA JUU

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| **UMATAIFISHAJI WA MITAALA** | | | | |
| 1 | Kusimamia utekelezaji wa mitaala ya taifa ya elimu ya juu inayokidhi viwango vya kimataifa. | Idadi ya mitaala iliyosimamiwa na kutekelezwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu (TCU na NACTVET) |
| 2 | Kujengea uwezo taasisi za elimu ya juu kutengeneza mitaala na kufanya marejeo na maboresho ya mitaala yenye kuzingatia dhana, maudhui na mafunzo kwa njia ya vitendo katika viwango vya kimataifa. | Idadi ya taasisi zilizojengewa uwezo.<br>Idadi ya mafunzo yaliyotolewa.<br>Idadi ya mitaala iliyoboreshwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu (TCU na NACTVET) |
| 3 | Kuoanisha mitaala ya elimu ya juu iendane na viwango vya kikanda na kimataifa. | Idadi ya mitaala iliyooanishwa. | 2025-2026 | Taasisi za elimu ya juu<br>Taasisi rekebu (TCU na NACTVET) |
| 4 | Kuboresha na kuendeleza mitaala ya kujifunzia na kufundishia kwa njia ya masafa. | Idadi ya mitaala iliyo boreshwa na kuendelezwa. | 2025 - 2027 | Taasisi za elimu ya juu, Taasisi rekebu TCU/NACTVET/ NECTA) |
| 5 | Kutoa ithibati kwa taasisi za elimu ya juu kufundisha kwa kutumia mitaala yenye maudhui na viwango vya kimataifa. | Idadi ya taasisi zilizopewa ithibati. | 2025-2029 | Taasisi rekebu (TCU/ NACTVET/NECTA)<br>Taasisi za elimu ya juu |
| 6 | Kujenga uwezo wa taasisi rekebu kupokea, kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi. | Idadi ya watumishi waliojengewa uwezo.<br>Idadi ya vyeti vilivyo fanyiwa ithibati. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu<br>(TCU/NACTVET/ NECTA)<br>Taasisi za elimu ya juu. |
| 7 | Kuboresha mifumo ya ithibati kati ya taasisi rekebu na mabaraza ya kitaalamu. | Idadi ya mifumo iliyoboreshwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu<br>(TCU/NACTVET/ NECTA)<br>Taasisi za elimu ya juu. |
| 8 | Kuboresha miundombinu ili kuwezesha utekelezaji wa mitaala kwa njia mseto. | Idadi ya miundo mbinu iliyoboreshwa.<br>Taarifa ya utekelezaji. | Januari,<br>2026 - 2029 | Taasisi za elimu |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Kushirikisha jamii kuhusu umataifishaji na utekelezaji katika ngazi ya elimu ya juu. | Idadi ya mikutano na wanajamii.<br>Idadi ya watu walioshiriki.<br>Idadi ya matangazo | 2025 - 2029 | WyEST;<br>Taasisi za elimu ya juu;<br>Taasisi za Uwakala |
| **PROGRAMU ZA USHIRIKIANO NA TAASISI ZA ELIMU NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuweka kanuni na miongozo inayowezesha uanzishwaji na uendeshaji wa programu za ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi. | Idadi ya Kanuni na miongozo mipya.<br>Idadi ya Kanuni na Miongozo iliyoboreshwa. | 2026 | WyEST, Taasisi rekebu, Taasisi za elimu ya juu |
| 2 | Kuanzisha na kuhuisha mashirikiano na taasisi za elimu ya juu nje ya nchi yanayojikita katika kuendesha programu za ushirikiano. | Idadi ya Taasisi zinazoendesha Programu za ushirikiano. | 2025 -2029 | WyEST, Taasisi za elimu ya juu |
| 3 | Kujenga uwezo wa taasisi za elimu ya juu kuanzisha na kuendesha programu za ushirikiano. | Idadi ya programu za kujenga uwezo zilizoendeshwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za elimu ya juu |
| 4 | Kushirikisha wadau wato wanaohusika katika kuendesha programu za ushirikiano. | Idadi ya wadau walioshiriki. | 2025 - 2029 | WyEST,<br>Taasisi za elimu ya juu |
| **UDAHILI NA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI KUSOMA NCHINI** | | | | |
| 1 | Kuwezesha ofisi za umataifishaji za taasisi za elimu ya juu, taasisi za uwakala na taasisi rekebu kuratibu udahili wa wanafunzi toka nje ya nchi. | Idadi ya ofisi za umataifishaji, taasisi za uwakala na na taasisi rekebu zilizowezeshwa.<br>Idadi ya Mifumo ya udahili. | 2025-2029 | WyEST,<br>Taasisi za elimu ya juu,<br>Taasisi rekebu,<br>taasisi za uwakala |
| 2 | Kujenga uwezo wa taasisi rekebu kuthibitisha na kulinganisha vyeti vya kitaaluma kutoka taasisi za nje ya nchi. | Idadi ya wafanyakazi waliojengewa uwezo. | 2025-2027 | WyEST,<br>Taasisi rekebu, |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Kuboresha sera, kanuni na miongozo ya upatikanaji na usimamizi wa vibali/pasi za masomo na kufanya tafiti kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi. | Idadi ya sera, kanuni na miongozo iliyoboreshwa<br>Idadi ya vibali/pasi za masomo<br>Idadi ya vibali vya tafiti. | 2025-2029 | WyEST, Wizara za Kisekta, COSTECH |
| 4 | Kuweka utaratibu unaoruhusu wanafunzi kudahiliwa katika taasisi za elimu ya juu kwa vipindi tofauti ndani ya mwaka wa masomo. | Idadi ya vipindi vya udahili kwa mwaka. | 2025-2027 | WyEST,<br>Taasisi za Elimu,<br>Taasisi rekebu |
| 5 | Kutumia fursa za makubaliano ya kikanda ikiwemo ufadhili na ulinganifu wa ada katika jumuiya za kikanda. | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za elimu ya juu |
| 6 | Kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi katika programu za kimkakati. | Idadi ya programu za kimkakati zenye ufadhili.<br>Idadi ya wanafunzi wanaopata ufadhili katika programu za kimkakati. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za elimu ya juu |
| 7 | Kushirikisha taasisi za uwakala kudahili wanafunzi wa kimataifa katika taasisi za elimu. | Idadi ya hati za makubaliano kati ya taasisi za uwakala na taasisi za elimu.<br>Idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa kupitia taasisi za uwakala. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu,<br>Taasisi za uwakala. |
| 8 | Kuboresha mifumo ya utangazaji wa programu na huduma zinazotolewa na taasisi za elimu ya juu. | Idadi ya njia za utangazaji zilizotumika.<br>Idadi ya programu zilizotangazwa.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa. | 2025-2029 | WyEST,<br>Taasisi za Elimu ya juu, Taasisi za uwakala, Balozi za ndani na nje ya nchi, |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili, Kingereza, lugha za nyingine za kigeni na lugha ya alama. | Idadi ya programu za lugha mbalimbali zilizoanzishwa.<br>Idadi ya taasisi za elimu zinazoendesha programu ya Lugha.<br>Idadi ya wataalamu wa lugha mbalimbali.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kwenye programu za Lugha mbalimbali. | 2025-2029 | Taasisi rekebu,<br>Taasisi za Elimu ya juu |
| 10 | Kuimarisha utaratibu wa wanafunzi wa kigeni kutembelea vivutio vya utalii Tanzania. | Idadi ya wanafunzi wa kigeni waliotembelea vivutio vya utalii. | 2025-2029 | Tasisi za elimu ya juu,<br>Mamlaka zinazosimamia vivutio vya utalii. |
| 11 | Kuimarisha ushiriki katika maonesho na mashindano ya taasisi za elimu ya juu kimataifa. | Idadi ya taasisi za elimu zilizoshiriki maonesho na mashindano kimataifa.<br>Idadi ya maenesho ya kimataifa yaliyoendeshwa. | 2025-2029 | Taasisi za elimu ya juu, Taasisi za uwakala,<br>Balozi za Tanzania nje ya nchi. |
| **UDAHILI WA WANAFUNZI KUSOMA NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa kitaifa wa kuratibu fursa za ufadhili wa wanafunzi. | Mwongozo kukamilika. | Oktoba, 2025 | WyEST |
| | | Taarifa ya usimamizi na utekelezaji wa mwongozo. | 2025-2029 | |
| 2 | Kuboresha utangazaji wa fursa za masomo zinazopatikana nchi za nje. | Idadi ya njia za utangazaji zilizotumika.<br>Idadi za fursa zilizotangazwana zinazopatikana.<br>Idadi ya wanafunzi wanaoshiriki. | 2025-2029 | WyEST, Balozi za ndani na nje, Taasisi za uwakala,<br>Taasisi za elimu ya juu |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Kushirikiana na taasisi za uwakala katika kupeleka wanafunzi nchi za nje. | Idadi ya Hati za makubaliano kati ya taasisi za uwakala na taasisi za elimu ya juu.<br>Idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa kupitia taasisi za uwakala. | 2025-2029 | Taasisi rekebu,<br>Taasisi za Elimu,<br>Taasisi za Uwakala wa Elimu |
| 4 | Kuboresha ushirikiano kati ya taasisi za ndani na za nje ya nchi. | Idadi ya hati za makubaliano zilizosainiwa.<br>Idadi ya wanafunzi wanaofaidika na makubaliano ya mashirikiano. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu,<br>Taasisi za Uwakala |
| 5 | Kuandaa semina na makongamano ili kujenga uelewa kwa wananchi kuona fursa za masomo nchi za nje. | Idadi ya semina na makongamano yaliyoandaliwa.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu, Taasisi za Uwakala wa Elimu |
| 6 | Kuboresha na kuunganisha mifumo ya utoaji wa ithibati na utambuzi wa taasisi za elimu nje ya nchi. | Idadi ya mifumo iliyounganishwa. | Desemba, 2025 | WyEST, |
| | | Idadi ya ithibati zilizotolewa. | 2025-2029 | Taasisi za rekebu |
| **KUAJIRI WATAALAMU KUTOKA NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuboresha na kusimamia kanuni na miongozo ya ajira za wanataaluma na wataalamu wengine katika taasisi za elimu toka nje ya nchi. | Idadi ya Miongozo na taratibu iliyoboreshwa. | 2025 | WyEST, Wizara za Kisekta |
| | | Idadi ya taasisi zilizoajiri wataalamu wa nje.<br>Idadi ya wataalamu wa nje walioajiriwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu |
| 2 | Kuboresha taratibu za upatikanaji wa vibali vya kazi kwa wanataaluma na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi. | Idadi ya taasisi zilizoajiri wataalamu wa nje.<br>Idadi ya wanataaluma na wataalamu wa nje walioajiriwa kutoka nje ya nchi. | 2025-2029 | WyEST, Wizara za Kisekta, Taasisi za Elimu |
| 3 | Kuboresha stahiki za wanataaluma na wataalamu wengine kutoka nje ya nchi. | Idadi ya miongozo ya stahiki za ajira za wataalamu kutoka nje ya nchi iliyoboreshwa. | 2025 | Taasisi za Elimu |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya wataalamu kutoka nje ya nchi walionufaika. | 2025 - 2029 | Taasisi za Elimu |
| 4 | Kuboresha miundombinu ya taasisi za elimu ili kuvutia wanataaluma na wataalamu wengine wa kimataifa. | Idadi na aina ya miundombinu iliyoboreshwa.<br>Idadi na aina ya wanataaluma na wataalamu walionufaika. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu |
| 5 | Kuandaa programu za mafunzo ya lugha na utamaduni kwa wanataaluma na wataalamu wengine wa kimataifa ili kuwasaidia kuelewa na kuingiliana vyema na jamii za wenyeji. | Idadi ya programu za mafunzo ya lugha na tamaduni zilizoandaliwa.<br>Idadi ya wanufaika wa programu. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu |
| **MABADILISHANO YA WATAALAMU NA WANAFUNZI** | | | | |
| 1 | Kuboresha miundombinu ya taasisi za elimu ya juu ili kufikia viwango vya kimataifa. | Idadi ya taasisi zilizoboresha miundombinu.<br>Idadi ya wataalam na wanafunzi waliohusika katika mabadilishano. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu,<br>Taasisi za Elimu ya juu, Taasisi za uwakala |
| 2 | Kuratibu programu za masomo ya muda mfupi ili kuwawezesha wanafunzi kutoka nje ya nchi kushiriki programu za mabadilishano. | Idadi ya propgramu za muda mfupi.<br>Idadi ya Wanafunzi walioshiriki programu za muda mfupi. | 2025-2026 | Taasisi za Elimu ya juu |
| 3 | Kuongeza mabadilishano ya watahini kutoka taasisi za elimu ya juu za ndani na nje ya nchi. | Idadi ya watahini.<br>Idadi ya Taasisi zenye watahini kutoka nje ya nchi. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu |
| 4 | Kuongeza idadi ya wanataaluma na wataalamu wengine wa nje wanaoshiriki kufundisha programu za mabadilishano. | Idadi ya wataalamu kutoka nje.<br>Idadi ya Programu zilizofundishwa na wataalamu wa mabadilishano. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Kuboresha uratibu na ufanisi wa programu za mabadilishano ya elimu ya juu. | Idadi ya wataalamu kutoka nje walioshiriki tafiti na kufanya kazi kutokana na programu za mabadilishano.<br>Idadi ya wanafunzi waliohusika katika program za mashirikiano zilizoboeshwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu, Wizara na taasisi za kisekta |
| 6 | Kuboresha utaratibu wa kuingia na kutekeleza makubaliano ya mabadilishano ya wanafunzi, wanataaluma na wataalamu wengine. | Idadi ya Hati za Makubaliano na taasisi za elimu nje ya nchi.<br>Idadi ya wanafunzi walionufaika kutokana na makubaliano. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu, Taasisi za uwakala |
| 7 | Kuweka utaratibu wa programu za mabadilishano zinazojumuisha utalii wa elimu. | Idadi ya Programu zilizojumuisha utalii wa elimu zilizoanzishwa. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu, Taasisi za uwakala |
| 8 | Kuongeza rasilimali fedha ili kuwezesha programu za mabadilishano ya wataalamu na wanafunzi. | Fedha zilizotengwa kwa ajii ya mabadilishano.<br>Idadi ya Maandiko ya kutafuta fedha za Ufadhili. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu |
| | **MASHIRIKIANO KATIKA ELIMU, STADI, UTAFITI NA UBUNIFU** | | | |
| 1 | Kuanzisha na kutekeleza makubaliano ya ushirikiano kwenye maeneo ya ubobezi na umahiri. | Idadi ya makubaliano yaliyoanzishwa.<br>Idadi ya makuubaliano yaliyotekelezwa.<br>Idadi ya miradi ya ushirikiano. | 2025-2029 | WyEST na Taasisi za elimu ya juu |
| 2 | Kuboresha uwezo wa kuandika miradi ya kimkakati ili kuongeza ubobezi kwenye mafunzo, utafiti na ubunifu. | Idadi ya watumishi walioboreshewa uwezo, na Idadi ya miradi ya pamoja iliyopata ufadhili. | 2025-2029 | WyEST na Taasisi za elimu ya juu |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Kuboresha utaratibu na miongozo ya kutoa motisha kwa watafiti na wabunifu kuweza kubiasharisha na kuchapisha kwenye majarida yenye hadhi ya kimataifa. | Idadi ya watafiti waliopata Motisha.<br>Idadi ya Tafiti zilizofanyika kutokana na motisha.<br>Idadi ya matokeo ya utafiti iliyobiasharishwa. | 2025-2029 | WyEST, Taaasisi za elimu ya juu |
| 4 | Kujenga umahiri kwenye maeneo mahususi ya utafiti na ubunifu. | Idadi ya watafiti na wabunifu waliojengewa uwezo.<br>Idadi ya taasisi zilizojengewa uwezo. | 2025-2027 | WyEST na Taasisi za elimu ya juui |
| 5 | Kuwezesha watafiti na wabunifu wachanga kupata uzoefu wa stadi za tafiti na bunifu za viwango vya kimataifa. | Idadi ya watafiti na wabunifu wachanga waliowezeshwa. | 2025-2029 | WyEST na Taasisi za elimu ya juu |
| 6 | Kuboresha utaratibu wa kuchapisha matokeo ya utafiti na ubunifu kwa pamoja katika majarida ya kimataifa. | Idadi ya machapisho. | 2025-2029 | WyEST na Taasisi za elimu ya juu |
| 7 | Kuandaa na kushiriki makongomano ya kimataifa ya elimu, utafiti na ubunifu. | Idadi ya makongamano yaliyoandaliwa.<br>Idadi ya washiriki makongamano. | 2025-2029 | WyEST na Taasisi za elimu ya juu |
| 8 | Kujenga uwezo wa ubiasharishaji wa matokeo ya stadi, tafiti na bunifu kupitia vituo atamizi. | Idadi ya matokeo ya stadi, tafiti na bunifu kupitia vituo atamizi zilizojengewa uwezo wa ubiasharishaji.<br>Idadi ya watumishi waliojengewa uwezo. | 2025-2029 | WyEST na Taasisi za elimu ya juu |
| 9 | Kuboresha mifumo wa kumiliki haki miliki za matokeo ya stadi, tafiti na bunifu kwa pamoja. | Idadi ya haki miliki zinazomilikiwa kwa pamoja. | 2025-2029 | Taasisi za elimu ya juu na BRELA |
| **TAASISI ZA ELIMU NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuratibu uanzishaji wa taasisi za elimu (Chuo/kampasi/vituo vya mafunzo na utafiti) nje ya nchi. | Idadi ya vyuo, kampasi, au vituo vilivyoanzishwa.<br>Idadi ya programu zilizotangazwa. | 2027 - 2029 | WyEST, Taasisi za ithibati (TCU/ NACTVET), Taasisi za Elimu |

| | MKAKATI | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | MATARAJIO (TARGET) | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Kuvutia wanafunzi kupitia programu zinazolenga sekta za kipaumbele katika nchi husika. | Idadi ya programu kwenye sekta za kipaumbele zilizoanzishwa.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa. | 2026 -2029 | WyEST, Taasisi za Elimu |
| 3 | Kuanzisha kampasi/shule/chuo na vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi kupitia makubaliano ya ushirikiano na taasisi za elimu za nje ya nchi. | Idadi ya makubaliano ya mashirikiano.<br>Idadi ya kampasi za nje zilizoanzishwa.<br>Idadi ya programu zilizoanzishwa kwa makubaliano ya mashirikiano. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu |
| 4 | Kuweka utaratibu kwa wanataaluma na wataalamu wengine nchini kufundisha, kufanya utafiti, ubunifu na kufanya kazi katika kampasi/chuo/vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi. | Idadi ya wataalamu wa nchini waliopata fursa kufundisha na kufanya kazi katika nje ya nchi. | 2027-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu. |
| **TAASISI ZA ELIMU NJE NA NDANI YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuboresha miongozo na usimamizi wa kuanzisha kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti vya taasisi za elimu kutoka nje ya nchi. | Idadi ya miongozo iliyoboreshwa. | Septemba, 2026 | WyEST,<br>Wizara za kisekta, Taasisi rekebu |
| 2 | Kubainisha na kuendesha programu za kipaumbele za ufundi, stadi za kazi, kitaaluma, utafiti na ubunifu zinazohitajika ndani ya nchi. | Idadi ya programu za kipaumbele zilizobainishwa. | Julai, 2026 | WyEST, Taasisi rekebu, Taasisi za Elimu |
| 3 | Taasisi za elimu ya juu za nje ya nchi kuanzisha kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti vya ndani kupitia makubaliano ya ushirikiano na taasisi za elimu za ndani ya nchi. | Idadi ya makubaliano ya mashirikiano ya kuanzisha kampasi, vyuo na vituo.<br>Idadi ya kampasi zilizoanzishwa. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu, Taasisi za Elimu |
| 4 | Kuboresha utaratibu wa wanataaluma na wataalamu wengine nchini kuweza kufundisha na kufanya kazi katika kampasi, vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti nje ya nchi. | Idadi ya wataalamu wanaofundisha na kufanya kazi kwenye kampasi, vyuo na vituo vya nje ya nchi. | 2025 - 2029 | WyEST, Wizara za kisekta, Taasisi rekebu, Taasisi za Elimu |

## JEDWALI NA. 1 (c): MASUALA MTAMBUKA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **LUGHA YA KISWAHILI** | | | | |
| 1 | Kufundisha lugha ya Kiswahili kitaifa, kikanda na kimataifa katika ngazi zote za elimu. | Idadi ya watu waliofundishwa Kiswahili.<br>Idadi ya Taasisi za elimu zinazofundisha Kiswahili. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu |
| 2 | Kuboresha mitaala, mafunzo na utafiti wa lugha ya Kiswahili. | Idadi ya mitaala iliyoboreshwa.<br>Idadi ya taasisi yenye mitaala ya Kiswahili iliyoboreshwa.<br>Idadi ya taasisi zilizofanya mafunzo na tafiti kwa lugha ya Kiswahili.<br>Idadi ya wanafunzi walionufaika. | 2025-2029 | Taasisi za elimu ya juu |
| 3 | Kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa somo kwenye programu za kimkakati zenye ufadhili unaotolewa na serikali au taasisi za elimu ndani ya nchi. | Idadi ya wanafunzi waliofundishwa Kiswahili.<br>Idadi ya taasisi za elimu ya juu zinazofundisha program za kimkakati kwa kiswahili. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu |
| 4 | Kuandaa na kushiriki mashindano na makongamano ya kitaaluma ya lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani. | Idadi ya walioshiriki makongamano.<br>Idadi ya mashindano na makongamano shiriki.<br>Idadi ya taasisi za elimu ya juu zilizoshiriki makongamano. | 2025-2029 | WyEST,<br>Taasisi za elimu ya juu, Balozi za Tanzania nje ya nchi, Wizara za kisekta |
| 5 | Kuanzisha mashirikiano na taasisi za elimu nje ya nchi zinazofundisha lugha za kigeni. | Idadi ya Taasisi zilizoanzisha mashirikiano.<br>Taarifa ya utekelezazi. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu<br>Balozi za Tanzania nje ya nchi,<br>Taasisi za uwakala |
| 6 | Kuanzisha programu za mabadilishano ya wanataaluma na wanafunzi wa Kiswahili na lugha za kigeni. | Idadi ya programu zilizoanzishwa.<br>Idadi ya ya wanataaluma na wanafunzi waliohusika katika mabadilishano. | 2025-2029 | Taasisi za Elimu ya juu, Taasisi za uwakala, Wizara za kisekta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Kuweka miundombinu inayohitajika katika kujifunzia na kufundishia lugha. | Idadi na aina ya miundombinu iliyopo kwa ajili ya kufundishia lugha. | 2025-2026 | WyEST, Taasisi za Elimu ya juu, BAKITA |
| 8 | Kuweka kanuni na miongozo inayowezesha ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na za kigeni nchini. | Idadi ya kanuni na miongozo iliandaliwa kufundisha lugha za kigeni.<br>Idadi ya taassi za elimu ya juu zinazofundisha lugha ya Kiswahili na za kigeni nchini. | 2025-2026 | WyEST, BAKITA, Taasisi za Elimu ya juu |
| **MATUMIZI YA BALOZI ZA NDANI NA NJE YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuimarisha ofisi za uambata wa elimu katika Balozi nje ya nchi. | Idadi ya ofisi za waambata zilizoboreshwa. | 2025-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi |
| 2 | Kuboresha mifumo ya kubaini wanafunzi, walimu, wanataaluma, wataalamu wengine na taasisi mahiri na bobezi katika maeneo ya elimu, ufundi, stadi za kazi, kitaaluma, kitafiti na ubunifu. | Idadi ya wataalamu na taasisi zilizobainishwa. | 2025-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi, Taasisi za Elimu |
| 3 | Kuimarisha mahusiano kati ya taasisi za elimu ndani na nje ya nchi. | Idadi ya taasisi zilizoimarishwa. | 2025-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi, Taasisi za Elimu |
| 4 | Kuimarisha utaratibu wa ushirikiano na taasisi za uwakala. | Idadi ya wakala wa udahili wa wanafunzi.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kupitia Wakala. | 2025-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi, Taasisi za Elimu ya juu na mawakala. |
| 5 | Kuboresha mifumo ya ufuatiliaji mienendo na maendeleo ya wanafunzi ya kitaaluma na kijamii wanaosoma nje ya nchi. | Idadi ya miongozo ya ufuatiliaji wanafunzi, na idadi ya wanafunzi waliofuatiliwa. | 2025-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi, na mawakala |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **TAASISI ZA UWAKALA WA ELIMU NDANI YA NCHI** | | | | |
| 1 | Kuboresha miongozo na majukumu ya Taasisi za uwakala wa uandikishaji na udahili wa wanafunzi wa elimu ndani na nje ya nchi. | Idadi ya Miongozo iliyoboreshwa.<br>Idadi ya Taasisi za uwakala zinazoshiriki uandikishaji na udahili wa wanafunzi wa elimu ndani na nje ya nchi. | 2025-2026 | WyEST, Taasisi rekebu, Taasisi za Uwakala |
| 2 | Kuimarisha makubaliano ya ushirikiano kati ya wakala, wizara na taasisi za elimu. | Idadi ya hati za makubaliano kati ya taasisi za elimu ya juu na taasisi za uwakala.<br>Idadi ya Taasisi za uwakala zinazotekeleza makubaliano.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa ndani na nje ya nchi kupitia Taasisi za uwakala. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi za elimu ya juu, Taasisi za uwakala , Taasisi rekebu |
| 3 | Kuboresha mahusiano kati ya wakala na balozi za ndani na nje ya nchi. | Idadi ya Ofisi za Ubolozi na wakala zilizoboresha mahusiano.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika tassisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi kupitia taasisi za uwaka. | 2025-2029 | WyEST, Wizara za kisekta, Balozi, Taasisi za Uwakala |
| 4 | Kujenga uwezo wa mawakala kujiendesha kulingana na sheria, kanuni na taratibu za udahili wa wanafunzi. | Idadi ya Wakala walijengewa uwezo.<br>Idadi ya Taasisi za uwakala zinazotekeleza majukumu yao kulingana na sheria, kanuni na taratibu za udahili wa wanafunzi.<br>Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa ndani na nje ya nchi kupitia Taasisi za uwakala. | 2025-2025 | WyEST, Taasisi za elimu ya juu, Taasisi za uwakala, Taasisi rekebu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Kutumia mawakala kubaini programu na fursa zitakazo saidia kuendeleza vipaumbele vya nchi katika kudahili wanafunzi ndani na nje ya nchi. | Idadi ya taasisi za uwakala zinazotumika kubaini programu.<br>Idadi ya Programu na fursa zilizobainishwa.<br>Idadi ya programu na fursa zinazosaidia kuendeleza vipaumbele vya nchi katika kudahili wanafunzi ndani na nje ya nchi. | 2025-2029 | WyEST, Taasisi rekebu, Taasisi za elimu ya juu, Taasisi za Uwakala |
| 6 | Kuziwezesha taasisi za uwakala kufuatilia mienendo na maendeleo ya wanafunzi wanaosoma nje ya nchi. | Idadi ya taasisi za uwakala zilizowezeshwa.<br>Taarifa ya utekelezaji. | 2025-2029 | WyEST, Wizara za kisekta, Balozi, Taasisi za Uwakala |
| **UDAHILI WA WANAFUNZI KUTOKA NCHI ZENYE MAJANGA** | | | | |
| 1 | Kuboresha miongozo na taratibu za kupokea, kuandikisha na kudahili wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga. | Idadi ya Miongozo uliyoboreshwa na idadi ya wanafunzi waliodahiliwa. | Januari, 2026-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Ndani na Taasisi za elimu ya juu |
| 2 | Kuimarisha mifumo ya utambuzi wa sifa za elimu, uandikishaji, udahili na usimamizi wa wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga. | Idadi ya mifumo wa kijiditali wa kujisajili na kutathmini sifa za kitaaluma iliyoanzishwa. | 2025-2027 | WyEST, Taasisi rekebu, na taasisi za elimu ya juu, Wizara ya Mambo ya Ndani. |
| 3 | Kuingia makubaliano na taasisi zinazotoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga. | Idadi ya taasisi zilizoingia katika makubaliano.<br>Idadi ya wanafunzi waliopata ufadhili kwa kuingia makubaliano. | 2025-2029 | WyEST<br>Taasisi za elimu ya juu |
| 4 | Kuimarisha ushirikiano na Balozi pamoja na taasisi za kimataifa ili kuweka utaratibu wa kusimamia na kutatua changamoto za wanafunzi wanaotoka nchi zenye majanga. | Idadi ya changamoto zilizotatuliwa. | 2025-2029 | WyEST, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi, na Wizara ya Mambo ya Ndani |

# Marejeo


1. African Union Commission (2015). Agenda 2063. The Africa We Want.
2. Association of African Universities (AAU) Strategic Plan 2020-2025.
3. URT. (2024).Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 na Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo ya Taifa 2011/12 hadi 2024/25 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26).
4. CCM. (2025).Ilani Chama cha Mapinduzi 2025 - 2030.
5. Jumuiya ya Afrika Mashariki (2008).Itifaki ya kuanzishwa kwa soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2008.
6. Mkakati wa Baraza la Vyuo vikuu vya Afrika Mashariki wa 2021-2026.
7. Mkakati wa Chama cha Vyuo Vikuu vya Kanda ya Afrika Kusini wa mwaka 2008-2012 na mwaka 2024-2028.
8. Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu ya Juu wa Finland (2009–2015).
9. Mkakati wa Umataifishaji wa Elimu ya Juu wa Jamhuri ya Czech (2021).
10. URT.(2023).Sera ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania ya mwaka 2014, toleo la 2023.
11. Sera ya Umataifishaji ya Afrika Kusini ya mwaka 2019.
12. UDOM (2024).Sera ya Umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dodoma.
13. Tanzania Commission for Universities. (2019). Handbook for Standards and Guidelines for University Education in Tanzania 3rd Edition 2019.
14. UDSM.(2022).University of Dar es Salaam Internationalization Policy 2022.
15. Itifaki ya elimu na mafunzo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya 2000.

**WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Mji wa Serikali
Mtumba - Mtaa wa Afya
S.L.P 10
40479 Dodoma, Tanzania**

**info@moe.go.tz
www.moe.go.tz**